# *Muhuri Wa Kweli Wa Pasaka*

Ibada ya mapema ya mapambazuko, ambapo Ndugu Neville alituhubiria ujumbe mzuri sana juu ya—ya ibada ya Pasaka.

2 Na sasa ninajua ni vibaya sana kulazimika kusimama, nafasi ye—yetu ya kuketi hapa ni ndogo sana. Nao ndio kwanza waniulize kama wanaweza kufungua upande wa nyuma hapa na kuwaweka watu katika chumba cha kubatizia. Nikasema, "Hapo ni mahali pazuri pa kuwaweka." Hapo palikuwa ni mahali pazuri sana kwao. Wao, kwa hiyo watavuta mapazia katika dakika chache, na kuwa, nafikiri watasimama tu kandokando ukingoni. Sijui kama wako ama hawako, ninaona kimejaa maji, kwa hiyo karibu sana itawabidi kusimama juu ya ubao. Lakini ninaona wanaandaa baadhi yake sasa, kwa hiyo labda watakifungua katika dakika chache.

3 Sasa, Pasaka ni siku kuu kwetu sote, tunapenda Pasaka sana! Na sasa tutajaribu kutowaweka kwa muda mrefu kupita kiasi, maana chini ya hizi hali.

4 Ila ningetaka kufanya tangazo moja tu ama mawili, na hilo ni kwamba ibada ze—zetu zinaanza Jumapili ijayo, sasa, kwenu watu wa nje ya mji. Zinaanza katika Bloomington, Illinois, kwenye vi—viwanja vya Chuo cha Methodisti kule. Nao wataendelea kote, Jumapili hadi Jumapili. Ndipo kutakuwako na ki—kiamshakinywa cha wahudumu. Halafu ninapaswa kulizungumzia kundi la wanafunzi, humo chuoni, asubuhi moja, na kutakuwako na kiamshakinywa kule, nasikia.

5 Ndipo juma linalofuata, baadaye, hiyo ni tarehe ishirini na tatu hadi Ju—Jumapili ya mwisho. Ama ni nini hiyo? [Ndugu Neville anasema, "Kuna kijikaratasi juu yake, moja kwa moja pale, ndugu."—Mh.] Loo, naam. Vema, tayari imetangazwa basi, wanajua habari zake. ["Niliitangaza."] Naam, bwana, hilo ni sawa, vema. Chicago, sasa kumekuwako na . . . ndivyo nasikia kutoka jana usiku, hawawezi kupata Ukumbi wa Lane Tech, kwa hiyo itakuwa ni ukumbi yapata tu mwendo wa dakika kumi kwa gari kutoka Lane Tech. Kutakuwako na ukumbi mwingine, ninavyosikia. Hakika, labda watakuwa na alama kule zikiwaelekeza kwenye . . . mahali huo mkutano utakapokuwa.

Kisha tutapanda juu, British Columbia. Na halafu, kwenye Julai mosi, hadi nne, huko Miami, Florida.

6 Kwa hiyo basi ni kushangaa juu ya mkutano mkubwa wa hema, kwamba kama huo ukija, ninataka kweli kuwa kule ili . . . ninyi nyote mnaoweza, huko Washington, DC, kwenye mji mkuu, kwa ajili ya m—mkutano. Utakuwa ni mkutano wangu wa kwanza wa hema, mwajua, ambapo Bwana aliniahidi Yeye angekutana nami katika mahali padogo mkutanoni. Na

kwamba wanaupanga huo sasa, walitupigia simu wakatwambia, wafanyabiashara kule, ya kwamba ama watapata Ukumbi wa Mikutano, ambamo tulihubiria, au wapige hema kubwa. Basi mara aliposema "hema kubwa," kitu fulani kwa namna fulani kikanikumbusha, huenda ikawa huko ndiko ule mkutano utakakokuwa, bungeni. Kwa hiyo hilo ni zuri, zuri sana. Kwa hiyo tutalishughulikia hilo, na kuwajulisha baadaye kidogo, kadiri Roho Mtakatifu anavyoongoza njia.

7 Sasa ninaamini wana watoto wachanga hapa, waliotoka nje ya mji, ambao walitaka kuwekwa wakfu kwa Bwana. Sasa, hii, watu wengi huwanyunyizia, na kadhalika. Na hilo ni sawa kabisa, sina neno dhidi ya hilo. Hata hivyo, kunyunyizia si la Kimaandiko, kwa mtoto mchanga ama mtu mzima, mnaona. Kunyunyizia ni utaratibu tu wa ki—ki—ki—kikanisa ambao umechukuliwa, kwanza na kanisa Katoliki, kisha ukapokezanwa kupitia Uproterstanti. Bali hakuna Maandiko ya kumnyunyizia mtu mzima ama mtoto mchanga. Na kwa kuwa sisi tunapenda kudumu moja kwa moja na Maandiko, kwa karibu tu tuwezavyo, katika Biblia waliwaleta watoto wadogo kwa Bwana wetu, na Yeye akawainua juu, akawachukua mkononi Mwake na kuwabariki, na kusema, "Acheni watoto wadogo waje Kwangu." Sasa hivyo ndivyo tunavyojaribu kufanya, kuzifuata Amri za Bwana kwa njia hiyo. Nasi tunawaleta wazee wa kanisa, na kusimama kuwazunguka na kuwaweka wakfu hao watoto kwa Bwana.

8 Kama mpiga piano wetu atacheza wimbo wetu, *Waleteni*. Vema. Basi hao mama walio na watoto wadogo, watakuja, wasimame mbele. Ndugu Neville na baadhi ya wazee watasimama pamoja nami hapa, wakipenda, nasi tutawaweka wakfu watoto hawa kwa Bwana.

> Waleteni, waleteni,
> Waleteni kutoka maeneo ya dhambi;
> Waleteni, waleteni,
> Waleteni watoto wadogo kwa Yesu.

9 Sasa huu ni utaratibu tu, wa akina mama kuwaweka watoto wao wakfu kwa Bwana. Na asubuhi hii ya Pasaka, ni wakati mzuri jinsi gani kwa ajili ya ubatizo ama kuwekwa wakfu, msimu huu wa mapema na wakati wa ufufuo. Hebu tuuimbe tena wakati wengine wakianza.

> Waleteni, waleteni,
> Waleteni kutoka maeneo ya dhambi;
> Waleteni, waleteni,
> Waleteni watoto wadogo kwa Yesu.

10 Sasa, enyi marafiki, ninajua wao, kila mmoja, ndiye mtoto mrembo kuliko wote ulimwenguni. Ninajua hivyo. Ninajua vema kuliko kusema jambo lingine lolote kulihusu hilo. Hiyo ni kweli. Na hivyo ndivyo mnavyopaswa kujisikia.

11 Wao ni hazina ndogo ambazo Mungu amewapa jukumu la kuwalea. Nami daima nimesema, na kutoa tamshi la namna hii kwa akina mama. Tunajua, zimeandikwa, zile Injili nne, Mathayo, Marko, Luka, na Yohana. Lakini kuna Injili ya tano, isiyoandikwa, hiyo ni mama. Yeye anawapata kabla Mafundisho ya Mathayo, Marko, Luka, na Yohana kuwapata. Kwa hiyo jukumu limewekwa juu yenu akina mama na ninyi baba, kuwalea watoto hawa kwa. . .kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Nami nina hakika hiyo ndiyo shauku ya moyo wako.

12 Tunawainua kwa Mungu, katika maombi, na kuwaweka watoto wenu wachanga wakfu kwa Kristo. Mimi pamoja na wazee tutasonga mbele, nanyi mtupe tu jina. Na sasa ninajua mke wangu kidogo ananionea wivu katika kazi hii maana. . .

13 Lisa Ann Mitchell. Loo! Lisa Ann Mitchell, hazina kwa mkono wa mtu yeyote. Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

14 Baba wa Mbinguni, kama watumishi Wako, tunamwinua mtoto huyu Lisa Ann Mitchell Kwako, katika Jina la Bwana Yesu. Tunamweka wakfu na kuyadai maisha yake kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Jalia aishi na kukua na kuwa mtu mzuri sana kwa Ufalme wa Mungu. Tunafanya hili, kwa kuwa, kwa sababu tumeagizwa na Bwana wetu. Katika Jina la Yesu Kristo tunaomba. Amina.

Mungu akubariki.

15 H. A., E. J. Junior. E. J. Junior, wakati akilala kidogo. Kwa hiyo hebu tuinamishe vichwa vyetu.

16 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuinulia Wewe jamaa huyu mdogo; tunaomba ya kwamba kama Yesu akikawia, utamfanya mtumishi mkuu wa Mungu. Mama anakupa Wewe. Na—nasi tunamkabidhi, katika Jina la Bwana Yesu, kwamba Wewe utambariki na makazi anamotoka. Jalia alelewe kwa utukufu wa Mungu, tunapomweka wakfu kwa Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki, dada, na mtoto wako mdogo. Kidogo mimi ni mwangalifu kwa kazi hiyo, maana sikuzote ninahofia nitawaumiza hawa jamaa wadogo.

17 Nitaacha, unaweza kumpata kama huyu. . .Huyu ni jamaa mdogo. Jina lake? Deborah Myers. Mtoto Deborah Myers, ana macho maangavu asubuhi ya leo. Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

18 Baba wa Mbinguni, tunakuletea Wewe, mtoto Deborah Myers, tunaomba baraka Zako juu ya mtoto huyu. Tunapomweka wakfu kwa Bwana, wakati baba na mama sasa wanamkabidhi, kama katika kumbukumbu la Bwana Yesu Yule aliyewabariki watoto wadogo, kasema, "Waacheni waje Kwangu," tunakukabidhi Wewe, mtoto Deborah, kwa ajili ya maisha ya utumishi, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

19 Sasa ni yupi kati ya hawa jamaa wengine wadogo? Vema, bwana. Sasa jamaa huyu mdogo, Sarah Ruth, mtoto Sarah Ruth Wheeler. Wheeler. Anapendeza.

20 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuletea Wewe mtoto huyu mchanga kipenzi ambaye amekabidhiwa mikononi mwetu kwa ajili ya kuwekwa wakfu. Nasi tunasimama na vichwa na mioyo iliyoinamishwa, kukushukuru Wewe kwa ajili yake, na kuomba ya kwamba Wewe utayabariki maisha yake kwa maisha ya utumishi Wako. Tunamkabidhi Kwako katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki. Yote yamekwisha sasa. Aliangalia nyuma, kama kwamba (kwangu) kusema, "Chochote kingine?" Vema.

21 Huyo hapo msichana mdogo mzuri. Sasa jina lako ni nani? Mica Ungren. Ni mtoto mzuri jinsi gani. U hali gani? Ana wasiwasi sana, anataka kujua kinachoendelea huku juu. Na tuinamishe vichwa vyetu.

22 Baba yetu wa Mbinguni, tunakukabidhi Wewe maskini mtoto huyu wa kupendeza kwenye asubuhi hii ya Pasaka, tukiwaleta watoto wadogo Kwako. Tunamweka wakfu kwa Bwana Yesu, kwa ajili ya maisha ya utumishi. Tujalie, Bwana, ya kwamba ataishi muda mrefu, hata kule Kuja kwa Bwana, ikiwezekana. Na umfanye utumishi Kwako, tunapomweka wakfu kwake . . . yeye Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

23 Jina lake ni nani? Loo, Melynda, mtoto Melynda Ungren. Wa—wanataka kukuona *huku*, Melynda. Wewe ni—wewe ni mrembo. Jamani! Na tuinamishe vichwa vyetu.

24 Baba Mungu, tunakukabidhi Wewe msichana huyu mdogo, katika Jina la Bwana Yesu. Tunamweka wakfu Kwako, maisha yake, kwa ajili ya maisha ya utumishi Kwako, Bwana, tunaomba ya kwamba utamlinda na kumfanya mmoja wa wajakazi Wako kukutumikia Wewe na kufanya kile ambacho amezaliwa kufanya. Tunamkabidhi Kwako, katika kuwekwa wakfu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

25 Maskini wasichana hawa wote warembo! Hebu tuone sasa . . . Huyu, loo, hapa, huyu ndiye. U hali gani? U hali gani asubuhi ya leo? Jina lake ni nani, sasa? Jane . . . Jamie Lynn Daulton.

26 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuletea Wewe maskini msichana huyu mdogo mzuri, nasi tunaomba ya kwamba Wewe utambariki. Nasi tunaomba, Bwana, ya kwamba utayabariki makazi ya watoto hawa. Jalia walelewe katika maonyo ya Mungu, kwa maisha ya utumishi Kwako. Tunakukabidhi Wewe maskini kipenzi hiki, tunapomweka wakfu kwa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Amina.

Mtoto wako mdogo anapendeza.

27 U hali gani? Vema, sasa, karibu unaweza kunishika, sivyo? Jina lake ni nani? Teresa Cabert. Angalia huku, Teresa. Hivi yeye si ni maskini mtoto mdogo mrembo? Hawa wote ni watoto wachanga warembo sana.

28 Baba yetu wa Mbinguni, tunakukabidhi Wewe huyu msichana mdogo mpendwa, ambaye mpendwa wake amemleta kwetu. Tunapomwinua mtoto huyu Kwako, tunamkabidhi kwa ajili ya maisha ya utumishi kwa Mungu. Tunamweka wakfu kwa utumishi wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Amina.

29 Mungu akubariki, dada, na ambariki mtoto wako tunapoomba. Macho madogo ya samawati; halafu ya hudhurungi. Jina lake ni nani? Cynthia, mtoto Cynthia. Angalia *huku,* Cynthia. Hayo macho madogo mazuri.

30 Baba yetu wa Mbinguni, tunakukabidhi Wewe msichana huyu mdogo asubuhi ya leo. Jalia aishi muda mrefu, na jalia awe mjakazi Wako. Mpendwa anamweka mikononi mwangu kwa ajili ya kuwekwa wakfu, ninamleta mbele ya hawa wazee na kumweka mbele za Mungu, na kumweka wakfu kwa utumishi wa Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Amina.

31 Sasa, kidogo huyu ni mdogo, pia. Sasa, Meda, unapaswa kuwa hapa juu kumshika huyu. Sikuzote ninahofia nitamvunja. James, James Bliss. Yeye anaonekana jamaa mdogo mwenye hekima sana, sivyo? Jambo ndilo hilo.

32 Baba yetu wa Mbinguni, tunakukabidhi Wewe mtoto James. Jalia awe kama yule ambaye jina lake linatoka, James katika Biblia, hapana shaka, ambaye alionyesha hekima katika wosia wa huduma ya Bwana. Ninaomba ya kwamba utambariki, na kwa ajili ya maisha ya utumishi Kwako. Yabariki makazi anamotoka, na jalia alelewe katika maonyo ya Mungu; tunapomweka wakfu kwa utumishi wa Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Amina.

33 Hakika ninapenda. . . Jina la msichana huyu mdogo ni nani? Njoo huku, kipenzi. Huh? Tammy Brown. Hebu. . . Loo, mtoto Tammy Brown. Mama yake na baba walibatizwa asubuhi ya leo. Msichana mwingine mrembo. Na tuinamishe vichwa vyetu.

34 Baba, tunakuletea Wewe mtoto huyu mdogo. Ningewazia ilikuwa ni kitu kama hiki wakati mama walipowaleta Kwako, wakati Wewe ulipokuwa hapa, safari ya duniani. Tunamweka wakfu Kwako, Bwana. Kama ninavyosikia, baba na mama yake walibatizwa asubuhi ya leo hapa, katika Jina hilo la thamani la Bwana Yesu. Basi, makazi yake yatakuwa ni sawa. Ninaomba ya kwamba utambariki na kumpa maisha ya utumishi. Tunapomweka wakfu kwa Mungu kwa ajili ya utumishi Wake, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana Wake. Amina.

35 Asante. Loo, ngoja, samahani, sikumwona huyu. U hali gani? Vema, ni mwanamume mzuri jinsi gani. Naweza kushika. . .

Ungejali? Sawa. Jina lake ni nani? Danny Johnson, Danny William Johnson. Loo, jamani, hata anaonekana kama mhubiri, sivyo?

36 Baba wa Mbinguni, tunakuletea Wewe mvulana huyu mdogo. Labda yeye ni mdogo sana kujua haya yote yanahusu nini, bali kuna Mungu Mbinguni Ambaye anaangalia chini na anajua jambo hili. Tunamkabidhi Kwako, Bwana, kama vile mama alivyomweka mikononi mwetu. Kwa imani tunakuja katika Jina la Yesu Kristo, na kumdai kama kumbukumbu ya neema ya Mungu, na kumweka wakfu kwa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ubarikiwe, kipenzi.

37 Tuliwapata wote? Sasa ni msichana mdogo mrembo jinsi gani anayekuja hapa! Hiyo ndiyo nguo ndogo nzuri sana ambayo umevaa, na kofia ndogo. Adler, Adler, Ellen Gail Adler, ni msichana mdogo mrembo jinsi gani.

38 Baba yetu wa Mbinguni, ninashikilia Kwako maskini hazina hii ya nyumbani, msichana mdogo aliyekuja ulimwenguni. Na mpendwa anamleta huku apate kuwekwa wakfu kwa ajili ya utumishi Wako, akijua ya kwamba siku hii ovu tunayoishi. Tunayadai maisha ya mtoto huyu kama kumbukumbu kwa Mungu. Nasi tunamweka wakfu kwa utumishi wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Amina.

Ubarikiwe, kipenzi.

39 Huyu hapa mvulana mdogo mhubiri, wawili. Kwani wao ni mapacha? Mitano na Minane. Jina la huyu ni nani? Johnny. Kutoka Richmond, kutoka Richmond, Virginia. Nilifikiri niliukumbuka uso wako. Tulikuwa na usaili pamoja. Wakati Bwana alipokuwapo. Nisingeweza kukukumbuka; niliujua uso wako wala nisingeweza kujua ulikuwa nani. Vema. Vema, tunajua yeye atakuja katika nyumba ifaayo. Jina lake ni John, Johnny.

40 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuletea Wewe maskini mvulana huyu, Johnny. Nasi tunaweka mikono yetu juu yake, kwa kuwa hivyo ndivyo Wewe ulifanya. Uliweka mikono Yako juu yao. Nasi tunambariki na kudai maisha yake kama kumbukumbu ya neema ya Mungu, tunamweka wakfu kwa utumishi wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Amina.

Ubarikiwe, mvulana mdogo.

41 Lewis, huyu ni Lewis.

Baba wa Mbinguni, tunakuletea Wewe huyu mvulana mdogo, Lewis. Naye baba anamleta mbele kwa ajili ya kuwekwa wakfu akatumike katika nyumba ya Mungu.

42 Wakati tukiwazia juu ya siku zilizopita, wakati Hana aliposhuka kwenda hekaluni, na kuomba, na Mungu akampa

mtoto mchanga. Ndipo akamrejesha mtoto huyo na kumpa Mungu. Hivyo ndivyo watu hawa wanavyofanya leo, kuwaleta watoto wao humu, hazina zao ndogo, kuwaweka wakfu. Na—naye na—nabii akamchukua, Baba, na kumlea maskini jamaa huyo, naye akawa nabii.

Sasa tunamweka wakfu mtoto Lewis asubuhi ya leo kwa utumishi wa Mwenyezi Mungu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ubarikiwe, mwanangu.

Hakika ni vema kuwaona huku chini kutoka Richmond, Virginia, asubuhi ya leo. Mungu awabariki.

43 Sasa hebu tuone, hakuna wengine? Vema. Loo, ni jamaa hao wadogo! Hamjui, mimi, huenda tumewaweka wakfu wamishenari wengi wadogo asubuhi ya leo, na mhubiri, hatujui. Hayo yote yako mikononi mwa Mwenyezi.

44 Ninataka kutangaza ya kwamba ibada usiku wa leo, hapa maskanini, ambako kutakuwa na ibada ya ushirika. Na iwapo hujawahi kuhudhuria moja ya ibada zetu za ushirika, pia tunaadhimisha kutawadha miguu.

45 Sasa, kunazo leso zilizowekwa hapa nipate kuziombea. Moja ni ya Ndugu Grimsley, ndugu yetu hapa kanisani. Sijui hizi ni za nani. Sisi hutuma hizi nje, mamia na mamia yake, kote ulimwenguni. Na sasa tutaninii. . .Ninataka kuziombea nikishaanza kuwaombea wagonjwa.

46 Ninataka kuzungumza kwanza, kwa muda kidogo tu, juu ya kuendelezwa kidogo kwa Ujumbe wa Pasaka. Na sasa kabla hatujalikaribia Neno la Mungu, hebu tumkaribie Yeye kwa maombi.

47 Baba yetu wa Mbinguni, tunashukuru mioyoni mwetu asubuhi ya leo kwa ajili ya asubuhi hii adhimu. Na zaidi ya hayo yote, tunashukuru kwa ajili ya hii kile inawakilisha, kule kufufuka na thibitisho lililotiwa muhuri la dini yetu, wakati Yesu Kristo alipofufuka kutoka kwa wafu, miaka elfu mbili iliyopita, na akarudi akajionyesha Mwenyewe kwa Kanisa Lake, yu hai milele. Baada ya miaka elfu mbili, sisi tuna furaha sana kuwa tungali tunafurahia ushirika huo pamoja na wanafunzi wa Kristo aliyefufuka! Tunaomba, Bwana, ya kwamba Uwepo Wake utasikiwa sana katika jengo hili asubuhi ya leo, mpaka kila mtu hapa ambaye hajaokoka atamkubali Yeye kama Mwokozi wao. Na wale ambao hawajajazwa na Roho Wake, jalia hii iwe ndiyo ile siku ambapo Roho Mtakatifu atafanya kazi iliyomalizika juu yao. Tunaomba ya kwamba Yeye, katika Upatanisho Wake mkuu ambapo aliwaponya wagonjwa, jalia aje karibu sana na watu, hata imani itajitokeza, Bwana, na kutawala kutokuamini kote, ambayo itawafanya wagonjwa na wanaoteseka kuondoka kutoka hapa wameponywa na ni wazima.

Tungeomba, Bwana, ya kwamba Wewe ungembariki yule sasa anayejiandaa kulielezea Neno Lako, juu ya ufufuo.

Mungu, wabariki wahudumu wote kila mahali, watoto Wako, watumishi Wako kote nchini, kote ulimwenguni.

48 Kisha uje, Bwana Yesu, upesi, kwa kuwa tunaona mawingu yakielea hewani, Bwana, ndipo tunajua ya kwamba kunalo jambo kubwa linalopanda juu. Waandae watu Wako. Loo, jalia wauchukue upanga wa Kweli, wajifunge silaha, wavute helmeti, wajifunge kwa Injili, na, zaidi ya mambo yote, wachukue ngao ya imani na kusonga mbele. Tujalie, Bwana, kwa kuwa mawingu ya vita yananing'inia chini. Tubariki leo sasa, kwa kuwa tunajua kwamba karibuni, tujuavyo sisi, tutamwona Yesu karibuni. Nasi tunaomba ya kwamba tutakuwa tayari kwenda wakati saa hiyo itakapowadia. Jalia tuiandae mioyo yetu, na kulimaliza hilo, kulimaliza kabisa, katika ibada ya asubuhi leo hii. Katika Jina la Yesu Kristo, nena nasi kupitia Neno Lako, Neno Lako ni Kweli. Amina.

49 Sasa kwenu ambao mngetaka kusoma nami katika Maandiko, fungueni Luka, mlango wa 24. Nami ninataka kusoma sehemu kubwa sana Yake hapa, Bwana akipenda, kupata msingi kwa yale ninayotaka kutumia dakika chache kwake. Na sasa mkitaka, kama kuna joto, nadhani, ama chochote kile, ninyi jistarehesheni kadiri mwezavyo, nami nitafanya upesi tu iwezekanavyo.

50 Nasi tunataka kusema jambo hili, kwamba hakika tunathamini uaminifu wenu wa kuja. Na wakati hiyo, ingawa watu hujaribu kusema ya kwamba Injili imepoteza mvuto Wake, na wakati watu wamekuja kutoka kote nchini kusimama katika mahali ambapo viungo vyao vinauma, kwa ajili ya ibada ya Bwana, ingali inaonyesha ya kwamba Mungu anao watu, na kungali kuna shauku moyoni mwao kumwona Mungu. Hata hivyo, Injili katika urahisi Wake, rahisi tu kama Injili ya Bwana wetu Yesu Kristo ilivyo, hata hivyo Ndiyo nguvu kuu kuliko zote zilizowahi kuipiga dunia, ni Injili ya Kristo. Nayo Injili si katika Neno pekee, bali ni kupitia kwa nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu. Na atujalie mambo haya tunaposoma sasa kutoka kwenye kifungu cha 36 cha mlango wa 24 wa Luka Mtakatifu.

> *Na walipokuwa katika*. . .*kusema habari hiyo, Yesu mwenyewe alisimama katikati yao, akawaambia, Amani iwe kwenu.*
>
> *Wakashtuka na* wakaogopa sana*, wakidhani kwamba wameona roho.*
>
> *Akawaambia, Mbona mnafadhaika? Na kwa nini mnaona shaka mioyoni mwenu?*
>
> *Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe: nishikenishikeni, mwone; kwa sababu*

*roho* haina *mwili na* mfupa, *kama mnavyoniona mimi kuwa nayo.*

*Na baada ya* wao*. . .kusema hayo, aliwaonyesha mikono yake na miguu yake.*

*Basi walipokuwa hawajaamini kwa furaha. . . wao. . .hawajaamini kwa furaha, huku* wakistaajabu, *aliwaambia, Mna chakula cho chote hapa?*

*Wakampa kipande cha. . .samaki* aliyepikwa, *na. . . sega.*

*Akakitwaa, akala mbele yao.*

*Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika torati ya Musa, na katika manabii na zaburi, kunihusu mimi.*

Ndipo *akawafungulia. . .akili zao wapate kuelewa na Maandiko.*

Ndipo *akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa, na kufufuka katika wafu siku ya tatu:*

*Na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la* dhambi, *kuanza tangu Yerusalemu.*

*Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya.*

*Na, tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu: lakini kaeni humu mjini Yerusalemu, hata* nyinyi *mpate. . .*mpaka *mvikwe uwezo utokao juu.*

*Akawaongoza mpaka. . .Bethania, akainua mikono yake akawabariki.*

*Ikawa katika kuwabariki,* alijitenga *nao, akainuliwa juu mbinguni.*

*Wakamwabudu, kisha wakarudi Yerusalemu wenye furaha kuu:*

*Nao walikuwa daima ndani ya hekalu, wakimsifu na kumbariki Mungu. Amina.*

Sasa kama nikiliita somo, ningetaka kuchukua hili, *Muhuri Wa Kweli Wa Pasaka.*

51 Jinsi nilivyokuja kuwazia kitu kama hicho, ilikuwa ni yapata juma moja lililopita nilikuwa nikienda zangu barabarani, kuingia Georgetown, mji mdogo chini ya New Albany hapa. Na kulikuwa na wavulana waliosimama mtaani, wakichukua sadaka kwa ajili ya mihuri ya Pasaka. Ndipo nikaanza kuwazia juu ya "muhuri wa Pasaka." Nami nikawazia, "Muhuri wa Pasaka ni nini? Hakika, unamaanisha mengi kuliko yale wavulana hawa wanachukulia sadaka, muhuri wa Pasaka."

Nami nikawazia, "Wao hufanya nini na mihuri kama hiyo, na pamoja na mchango unaochukuliwa kutoka kwake, ama kwa ajili yake?" Inawekwa, hakika, mihuri hii, juu ya nyaraka na kadhalika. Na ni matoleo ya hiari kwao, nayo hutumiwa kuwaweka watu hospitalini, walio na kifua kikuu, na kadhalika, na kuwaweka hospitalini, mahali pa raha, mpaka wamekwisha. Nami nikawazia, "Hakika, Pasaka ina kitu zaidi ya hicho, muhuri wa Pasaka. Ingemaanisha kitu fulani zaidi ya kumweka mtu hospitalini, kumstarehesha." Ambalo, hilo ni zuri sana, sasa, sina kitu dhidi yake. Hilo, Mungu awabariki, hilo ni jambo zuri sana. Lakini hata hivyo, inaonekana kana kwamba inapaswa kwenda mbele kidogo kuliko hapo, kwa kuwa Pasaka ilimaanisha mengi sana kwa Kanisa la Kikristo na kwa urithi wetu wa Kikristo, Muhuri wa ufufuo. Basi stampu ndogo ya posta, kitu kama hicho, inawezaje kuchukua mahali Pake? Isingeweza.

Kwa hiyo nikaanza kuwazia hilo, "Muhuri wa Pasaka ulikuwa ni nini?" Na hivyo ndivyo nilivyopata wazo hili la kuzungumza asubuhi ya leo juu ya Muhuri wa Pasaka.

52 Sasa Pasaka inayo, na mihuri, na kadhalika, iko kote katika Biblia. Tunaiona, ni ya kale kama Biblia, kote kote huko nyuma kufikia bustani ya Edeni tunaiona. Halafu basi tunaona ya kwamba chochote tunachokipata popote katika Biblia, hurudi kwenye Mwanzo. Yote yalianzia huko Mwanzo.

53 Halafu nilikuwa nikiwazia kwamba, kile nilichokuwa nacho niani mwangu kama Muhuri wa Pasaka, basi nikashangaa ni kwa nini Huo ulikataliwa hivyo, na jinsi ambavyo watu wangeukataa. Ni kwa nini ukahukumiwa hivyo? Nami nilikuwa nikiwazia basi kwamba Huo hauhukumiwi sikuzote, na si watu wote wanauhukumu.

54 Lakini Mungu amefanya njia hivi, kwamba mwanadamu amewekwa mahali ambapo analazimika kufanya uamuzi. Mwanadamu hawezi kuishi duniani pasipo kufanya uamuzi. Mungu hulazimisha jambo hilo kwake. Hana budi kufanya uamuzi. Basi kuna wakati ambapo inakubidi kufanya uamuzi wa masomo, inakubidi kufanya uamuzi wa yule utakayefunga ndoa naye, nawe huna budi kufanya maamuzi ya mambo mbalimbali.

55 Lakini katika bustani ya Edeni, ambako walikuwa na wavulana wawili pekee, uamuzi ulilazimishwa juu ya mwanadamu kufanya uamuzi. Nami nafikiri hutendwa apate kuonyesha jinsi alivyo hasa, kile alicho, kuonyesha kile alicho ndani yake. Sasa tunaona ya kwamba wakati uliwadia, kati ya Kaini na Habili, ambapo uamuzi ilibidi kulazimishwa, kwa sababu kwamba wakati wa kuabudu ulikuwa umewadia, na kila mmoja wa wavulana hao alikukwa ametoa njia ya kumwabudu Mungu.

56 Na kama mtaangalia, kati ya mema na mabaya kuna chembe moja ndogo tu ya tofauti. Nayo mabaya, katika siku za mwisho, yametabiriwa kwamba yangefanana sana na yaliyo mema, hata ingewapoteza walio Wateule kama yamkini, kati ya mema na mabaya.

57 Sasa, katika hao wavulana, wakati wakija kwenye madhabahu yao, na kuabudu. Sasa nilikuwa nikiwazia basi ni madhabahu mangapi asubuhi ya leo, katika makanisa ambapo maua mazuri yanawekwa madhabahuni. Na hilo ni sawa. Sina neno dhidi yake. Lakini hiyo inaonekana tu karibu ndiyo mwisho wa ibada, ni kuweka maua madhabahuni, ama—ama kanisa zuri, ama mapambo mazuri ama kitu fulani, na hiyo inaonekana kuimalizia.

58 Basi kwa namna fulani ilikuwa hivyo na Kaini, kwa sababu yeye alileta matunda ya kondeni, na kufanya ibada yake kwa Mungu, nayo ikakataliwa kwa sababu hakuja kwa njia ya kweli na sahihi ambayo Mungu alikuwa amemchagulia kupitia. Lakini alikuwa ametoa sadaka yake, na kufanya kila kitu kidini tu kama ndugu yake, bali alikataliwa. Na kwa sababu alikataliwa upande wa kiroho, basi ilisababisha wivu kuibuka ndani yake, kwa sababu alikuwa na tamaa.

59 Hiyo iko ndani ya mwanadamu, hawezi kujiepusha kuwa kile alicho, kwa kuwa amezaliwa katika hali hiyo. Mwanadamu amewakilishwa Mbinguni kama mwenye dhambi, na mwenye dhambi. Nilikuwa nikizungumza juu ya jambo hilo siku moja, ndipo mtu fulani akasema, “Basi hiyo si haki. Kama ninapaswa kuwakilishwa na kutotii kwa mtu mmoja, basi sina nafasi.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli, kwa sababu umezaliwa mwenye dhambi, bali umewakilishwa. Umehukumiwa kwa hukumu, kwa uwakilisho.”

60 Vema, basi, hilo linaonekana katili sana. Ila ligeuze upande huo mwingine, ndipo nasi tumechaguliwa tupate Uzima wa Milele, kwa uwakilisho. Ambapo mmoja alituwakilisha, kwa mauti; Mwingine alituwakilisha tupate Uzima wa Milele, kwa hiyo linaturudisha tena mbele ya—ya Kiti cha Enzi tena. Kila mwanadamu hurejea moja kwa moja mahali pale pale, kufanya chaguo letu.

61 Lakini tamaa hiyo ambayo sikuzote imekuwepo, mema na mabaya, mabaya yakijaribu kuyapindua mema. Ilianzia huko Edeni, nayo imeteremka kupitia nyakati. Imeteremka hata ikaingia kwenye mambo ya kitaifa. Imeshuka ikaingia kwenye mambo ya kanisa. Imeshuka ikayafikia maisha ya nyumbani. Tamaa, ikijaribu kutawala ama kuangamiza, ikijaribu kushinda, kusukumia nje. Nasi tunakiona kitu hicho kikitenda kazi kila mahali, na daima kimekuwa hivyo, jambo lile lile, likijaribu kubatilisha ama kushinda.

62 Kote katika Agano la Kale, Mungu, katika siku za manabii, huko nyuma. Ninayo kadhaa yameandikwa hapa chini, ambayo sitapata wakati wa kuyafikia. Lakini, Mungu, katika siku za manabii wa kale, katikati ya kila kitu, kama alivyofanya katika bustani ya Edeni, wakati Sauti ya kweli ya Mungu na ibada ya kweli ya Mungu ilipohukumiwa, na kutupwa nje na kuuawa, katika bustani ya Edeni, nayo Sauti ya Mungu ikanyamazishwa na tamaa na wivu, imekuwa hivyo kanisani tangu wakati huo, ikijaribu kuinyamazisha Sauti ya kweli ya Mungu.

63 Lakini kama ukiangalia, mara sauti ya Habili iliponyamaza, katika mauti, Mungu alimwinua Sethi kuchukua mahali pake. Ambalo halikuwa kitu ila kitangulizi cha Pasaka, kitangulizi cha ufufuo, ama kibadala mpaka ufufuo ulipokuja. Hilo liliendelea kwa kitambo kidogo, kote kupitia Agano la Kale tunaliona likiendelea. Manabii, Mungu aliidumisha Sauti Yake hai kwa manabii. Walinena Neno la Mungu; nao wakawapiga mawe. Na mara walipompiga mawe mmoja na kumwondolea mbali, Mungu angemwinua mwingine. Nao wangempiga mawe huyo na kumwondolea mbali, Mungu angemwinua mwingine. Sikuzote amemdumisha hai shahidi Wake. Kote katika nyakati Yeye ameidumisha Sauti Yake hai mbele za watu, kote kote tangu Edeni.

64 Na sasa tunaona, mara Kaini alipotambua ya kwamba alikuwa amefanya yale aliyofanya, vema, aliondoka Uweponi mwa Mungu, naye akatiwa muhuri mbali na Mungu, kwa alama iliyowekwa juu yake. "Akatoka," Biblia ilisema, "akatoka kwenye bustani ya Edeni, akatoka kwenye malango ya bustani, mashariki mwa Edeni." Akatoka, ametiwa muhuri, ametiwa alama, akatoka Uweponi mwa Mungu. Ni kitu cha namna gani!

65 Ni kitu cha ajabu jinsi gani, kwamba Kaini, kwa sababu ya wivu, na kwa sababu ya kutotaka kupatanishwa na Mungu kwa njia ile ile iliyotolewa aliyopitia ndugu yake. Mungu alimwambia Kaini, "Kama utaabudu kama Habili, utafanya vema."

66 Lakini Kaini ni kama alisema, "Hizi ndizo nimeweka pamoja. Hizi ndizo nilizo nazo, hizi ndizo ninazotoa. Zichukue hizi ama uziache, lolote utakalo, jichagulie tu Mwenyewe."

67 Sasa huo kidogo ndio mtazamo wa watu wakati wote, katika maisha ya kanisa, katika maisha mengine. "Kama. . . " wao wanasema, "Ninaenda kanisani. Ni—ni—ninalisaidia kanisa, na—nafanya hivi. Kama Mungu hawezi kukubali hayo, hayo ndiyo mazuri kuliko yote niwezayo kufanya." Mnaona? Bali bado hayo siyo Mungu anayohitaji. Mungu hahitaji hayo.

68 Mungu anahitaji nji—njia iliyowekwa. Yeye ameiweka njia, Naye anakuhitaji ukubali ile Yeye ameweka, unaona. Yeye hahitaji usaidizi wetu katika kumwambia Yeye la kufanya na jinsi ya kulifanya. Yeye ameweka njia kwa ajili yetu kufanya, na mambo tunayopaswa kufanya, na jinsi tunavyopaswa

kuyafanya, wala Yeye hahitaji mawazo yetu ndani yake hata kidogo. Hatupaswi kuja jinsi hiyo. Lakini tunaona ya kwamba watu wanaelekea kufanya hivyo, kote katika nyakati. Lakini Mungu alidumisha Sauti Yake hai kwa manabii Wake, na kadhalika, kote katika wakati wakati Yeye akija. Nasi tunaliona siku hizi.

69 Nasi tunaliona katika siasa. Ninayo mambo fulani yamewekwa hapa kuhusu siasa, jinsi ambavyo tungeona hata katika siku hizi mahali tulipo, kwamba watu wameuza haki zao za mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya siasa. Na kama hakuna mmoja wenu aliyepata kuchukua kanda hiyo niliyolizungumzia, huko Middletwon, Ohio; Jumapili, juma moja lililopita; juu ya Yezebeli na Ahabu, laiti ungaliisikiliza wakati mmoja. Na jinsi ambavyo hili taifa, kwa sababu ya tamaa, na dola chache za ziada, na wa—wazo linalopendwa na watu zaidi, wao kabisa wamemwuza Kristo kabisa kama tu Yuda alivyofanya miaka elfu mbili iliyopita, kwa vipande thelathini vya fedha. Loo, ni jambo la ajabu sana, kuwazia ya kwamba hali ambayo iko miongoni mwa taifa hili na watu hawa siku hizi! Kuwazia ya kwamba miaka mingi iliyopita, kamwe wasingalifanya kitu kama hicho. Lakini siku hizi wao ni wenye tamaa sana, wakijaribu kupata pesa nyingi zaidi, wakijaribu kupata nyakati zilizo rahisi. Sasa hiyo ni, bila shaka, si Ukristo.

70 Mkristo haombi apate mambo ya rahisi. Sisi si. . .Kunazo ahadi nyingi sana siku hizi zinazofanywa miongoni mwa Wakristo, wahudumu wengi sana huwaahidi watu kitu cha uongo, "Kama tu utamjia Kristo, shida zako zote zimetatuliwa." Nakwambia, unapomjia Kristo ndipo zinaanza. Hapo ndipo unapovaa nguo rasmi na kuchukua bunduki, na kuingia kwenye uwanja wa vita. Barabara hii ya Kikristo si rahisi. Ni vita tangu saa ile ile unapoanza, mpaka roho yako itakapowekwa huru na mauti. Huko kwenye pikiniki. Uko kwenye viwanja vya vita. Na kwa hiyo tumeahidiwa mambo.

71 Nami ninakuwa, wakati mwingine, ninachukia kusema jambo hili, bali ninalimaanisha kutoka moyoni mwangu, ya kwamba ninaduwazwa ninaposikia mambo mengi sana kuhusu imani ya ajabu-ajabu, dini ya ajabu-ajabu. Na kila kitu siku hizi kimekuwa kitu fulani cha a—ajabu-ajabu. Ni—ni mtu wa ajabu-ajabu. Nayo televisheni imefungua njia kupitia wanaanga, na kadhalika, na lundo la upuuzi, ajabu-ajabu. Loo. Nao wanayaleta hata kwenye uponyaji wa Kiungu siku hizi, uponyaji wa ajabu-ajabu. Sasa, Mungu hana mambo kama hayo. Wao wanawaleta watu, mara nyingi, jukwaani, nao ni watu wenye kipaji, hapana shaka, ila wanaelewa Injili vibaya, wanawapaka mafuta, na kuomba, na kusimama hapo, na kuwatikisa mpaka kitu fulani kinatukia; wanaponywa. Na labda mtu huyo anaishi katika dhambi, nao wanarudi huko nje na wanaona unarudi moja kwa moja juu yao tena. Labda

walikuwa chini ya mhemko wakati huo, ambapo imani ya Mungu ambayo walikusanya iliwaponya, bali wanapoenda miongoni mwa wasioamini, unarudi tena. Utafanya hivyo kila wakati.

Kile tunachohitaji leo hii ni uponyaji wa Kiungu, ni maamuzi dhahiri kwa ajili ya Kristo! Kweli.

72 Nilikuwa nikisoma barua hivi majuzi tu niliyotumiwa na Shirika la Kilutheri, huko Ujerumani, ambako ndu—ndugu mmoja alikuwa akikaa, na kufanya ibada ya uponyaji huko Ujerumani, akidhaminiwa na kanisa la Kilutheri na Wapentekoste, na kadhalika. Nayo nakala hii ya barua hii iliandikwa: "Naye akasema, 'Mnahubiri huo uponyaji wa Kiungu; ya kwamba yote iwapasayo kufanya ni, unawawekea mikono, nao wanahisi kitu fulani, na wanaponywa.' Akasema, 'Bila shaka ninatofautiana nanyi.' Akasema, 'Basi vipi kuhusu mtoto Deborah Stadsklev wakati alipokufa huko juu? Mtoto mzima kabisa, mwenye afya siku moja, halafu saa chache baadaye alikuwa amelala mauti. Nanyi nyote mkaenda huko, na mkaomba, na mkamtikisa, na kumpaka mafuta, na kila kitu, kwa ajili ya uponyaji, wala hapakuwapo na uhai wowote. Huyo mtoto mchanga alilala pale.' Kasema, 'Halafu wakamwandikia Ndugu Branham barua ya simu, na yeye hakusema kitu mpaka alipopata uamuzi dhahiri kabisa kutoka kwa Mungu, ndipo basi akaja katika Jina la Bwana Yesu, kusema Ne—Neno.'"

73 Sasa hilo ndilo tunalohitaji, kupata uamuzi dhahiri kabisa kutoka kwa Mungu. Hiyo ndiyo sababu hatuna budi kuja. Hiyo ndiyo sababu tunabatiza katika Jina la "Yesu Kristo," ni uamuzi dhahiri kabisa kutoka kwa Neno la Mungu. Hiyo ndiyo sababu tunakaa pamoja na mambo tufanyayo, kwa sababu ni Maagizo ya Mungu na Injili ya Mungu. Nasi hatuna budi kukaa Nalo jinsi tu lilivyoandikwa. Kama unakubalika, kama unachukiwa, kama haidhuru ni kitu gani kinachotukia, hilo halina uhusiano wowote Nalo. Mungu anataka maamuzi dhahiri kabisa. Nawe unawezaje kufanya hivyo wakati unajua kwanza umekosea? Huwezi kuwa na uamuzi dhahiri kutoka kwa Mungu. Unawezaje kuja na kuomba uponyaji wa Kiungu wakati ukijua ya kwamba moyo wako hauko sawa na Mungu, kumtumikia? Unaona, unataka kurudi na kufanya mambo yaliyo katika ulimwengu. Kamwe hutaponywa namna hiyo, unaona. Huna budi kuwa safi mbele za Mungu, na kuyaweka maisha yako na moyo wako wakfu kwa Mungu, na ndipo Mungu ataponya. Nao ni wa kudumu basi, maana imani yako imetiwa nanga.

74 Lakini ni katika, tunaona tamaa hiyo, hata hivyo, kanisani, na katika siasa, na katika mambo ya kitaifa. Taifa moja, angalieni hapa chini Afrika sasa, yale yanayoendelea. Angalieni, kwa sababu ya tamaa, angalieni kile kimetendeka huko chini sasa katika Afrika; sio huko tu, bali kote ulimwenguni, kila mahali, kwa maana mwanadamu anataka kuwa mtu fulani.

Wao, haya ndiyo yote waliyo nayo, ni papa hapa duniani, ama, wanaishi jinsi hiyo.

75 Kama haya ndiyo yote niliyokuwa nayo, ningekuwa mtu mwenye mashaka. Ninautazamia Mji ambao Mjenzi na Mbuni wake ni Mungu. Huko ndiko tunakoweka hazina zetu, kwa kusudi hilo.

76 Wana wa Kaini, ama hasa wana wa Shetani, wao ni wana wa Shetani kwa sababu Kaini alikuwa ni mwana wa Shetani. Na kwa hiyo, basi, wana wa Kaini siku hizi. Nanyi mnasema, "Una hakika na hilo, Ndugu Branham?" Naam, nina hakika. Nina hakika kabisa na hilo. Kwa kuwa . . . sikilizeni.

77 Yesu, wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye upesi aliwaambia hao viongozi wa dini ya kwamba, "Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi." Hata hivyo walikuwa ni watauwa, na walikuwa ni wa kidini, na walikuwa ni wanachuoni, nao walikuwa na majengo makubwa, walikuwa na makanisa makubwa, nao walikuwa na utaalamu mwingi, na ukuhani, na utaratibu, na kadhalika, bali walikosa kutambua Kristo alikuwa ni nani. Walikosa kuishika siku yao.

78 Na kama walivyofanya wakati huo, ndivyo wafanyavyo sasa, vile vile hasa. Wanakosa kutambua siku tunayoishi, na mambo ambayo Mungu anafanya. Sasa tunaona basi, wangeweka . . . kama hao viongozi wa kidini . . .

79 Sasa hili hapa! Kama viongozi hao wa dini katika siku hiyo waliitwa wana wa ibilisi, tunajua basi ya kwamba ibilisi, hapo mwanzo, alikuwa ndiye aliyemvuvia Kaini kumtesa ndugu yake na kumwua. Hilo ndilo jambo lile lile lililotukia kwa hao viongozi waliomtesa Yesu Kristo na kumwua. Walilazimika kufanya uamuzi vile vile tu kama walivyolazimika huko nyuma katika bustani ya Edeni. Walilazimika kufanya uamuzi, "Vema, vipi kuhusu Hili?" Wana wa Kaini, wana wa Shetani.

Mnasema, "Hilo linaenda kwa mataifa?"

80 Wakati Shetani alipompandisha Yesu juu ya ule mlima apate kumjaribu, alimwonyesha falme zote za ulimwengu. Sasa, hiyo ilikuwa ni zote zilizokuwako na zote zitakazokuwako, falme zote za ulimwenguni. Naye akasema, "Hizi ni zangu, nami ninafanya nazo lolote nitakalo. Ninaweza kuwafanya wapigane, ninaweza kuwafanya wafanye *hivi* ama chochote kile." Naye alidai falme za ulimwenguni, kwa hiyo tunaweza kuona jinsi tamaa na ubinafsi unavyoingia katika siasa. Mnaona? Tunaweza kuona basi mahali ulipo kanisani na katika viongozi wa kanisa, ambapo tamaa na ubinafsi unapoingilia kanisani.

81 Sasa angalia maskini tamaa iyo hiyo ya kale iliyoanza kwenye bustani ya Edeni, ambayo ilimtia mmoja muhuri mbaya, na kumtia huyo mwingine Muhuri mzuri, ikaja moja kwa moja kufikia kwenye nyakati za Bwana wetu Yesu. Wakati Yeye alipokuwa hapa duniani, alifanyiwa mashtaka

na yale yaliyoitwa "haki," mahakama ya haki. Hiyo ilikuwa ni dhihaka dhalimu jinsi gani! Hapakuwapo na jambo moja wangaliweza kupata dhidi Yake. Huo ulikuwa ni upande wa siasa. Wasingeweza kupata chochote dhidi Yake. Zaidi sana hata Pilato, mwenyewe, akasema, "Sioni hatia ndani Yake."

82 Ndipo linakuja kanisa. Wanalazimika sasa kufanya uamuzi. Baada ya ulimwengu wa kisiasa kumweka huru, kushirikiana na roho ile ile iliyokuwamo kanisani, iliyokuwamo katika siasa; kuonyesha ya kwamba kama Shetani alipoteza vita vyake hapa, angali alikuwa na kitu fulani akiba, angerejea moja kwa moja kanisani. Nao wakamsulubisha, kwa sababu walilazimika kufanya uamuzi. Nao wakasema, "Tupe Baraba badala ya Yesu." Unaona jinsi walivyofanya?

Liko moja kwa moja mbele ya macho yetu leo, jambo lile lile, na limekuwa na daima litakuwa, kulazimika kufanya uamuzi!

83 Sasa, wakati walipolazimisha uamuzi huo, Pilato alijua moyoni mwake ya kwamba wakati alipowafungulia... alipomwachilia Yesu kwa kanisa, ya kwamba yeye alijua kanisa ndilo lililomleta Kwake apate kusulubiwa; na kama alimwachilia arudi kwa kanisa, kanisa lingemsulubisha. Kwa hiyo, Pilato hana udhuru! Alichukua maji akajaribu kuiosha Damu ya Kristo kutoka mikononi mwake, bali hawezi kufanya hivyo.

84 Tangu wakati huo, hapa Uswidi, ama Uswisi, hasa, ambapo Pilato alikutana na mwisho wake miaka kadhaa baadaye, akaingia wazimu, akashikwa na kichaa, akajitupa katika shimo la maji akafa. Kuna simulizi inayosema ya kwamba, "Saa tisa alasiri, kwamba maji ya samawati hutoka chini ya kidimbwi hicho." Watu hukusanyika hapo kutoka kote ulimwenguni kuyaangalia. "Saa tisa, hayo maji yanayoonekana ya samawati, ya nili hutoka chini ya mahali fulani, na kutikisika juu ya hayo maji kisha yanarudi chini, kuonyesha ya kwamba hakuna maji yanayoweza kuosha Damu ya Yesu Kristo kutoka kwa mikono ya mtu yeyote." Yeye ana hatia!

85 Na kila mtu ambaye Kristo amepata kuweka mikononi mwako, hakuna kitu kinachoweza kumwosha atoke hapo. Kuna jambo moja tu la kufanya, ni kulikubali, kuliamini.

86 Wana wa Shetani, wana wa Kaini, wanawatesa wana wa Mungu, wanawaua. Hivyo ndivyo walivyomfanyia Habili. Hivyo ndivyo walivyomfanyia Yesu. Hivyo ndivyo walivyowafanyia manabii. Hilo ndilo lililo ndani yao kufanya tena, nao watalifanya mara tu barabara itakapofunguliwa kwao kufanya hivyo.

87 Kumbukeni, kwa namna fulani tumeingilia na kujipumbaza na mambo, na kuwaondoa watu kwenye barabara ya Injili na ya historia, ya yale yatakayotukia. Na hapa tunakabiliwa nalo tena, papa hapa katika taifa letu, na hakuna kitu tunachoweza

kufanya kulihusu. Lakini unasema basi, "Ndugu Branham, sababu yako ya kuzungumza dhidi ya hilo ni nini?" Si zaidi ya vile ningaliweza kuikomesha dhambi; ninaweza kuweka sauti yangu dhidi yake. Na hivyo ndivyo vile hasa ninavyofanya sasa dhidi ya dhambi, na dhidi ya jambo lililo baya. Tumefanya makosa, nasi tutavuna yale tuliyopanda, kweli kabisa.

88 Tangu Middletown, walikuwa na—na kusikia kesi. Wakamleta kasisi, mhubiri wa Kibaptisti, na mhubiri wa Kipresbiteri, pamoja, kushauriana juu ya mfuko wa fedha za shule. Naye huyo kasisi akakubali kwamba Waprotestanti walilipa kodi kama Ka—Katoliki, na—na kwamba fedha hizo zinapaswa kupewa pande zote mbili, ndipo akasema, "Kile tunachopaswa kufanya ni kufanya shule moja, shule ya Katoliki." Loo, hakika, wawapate watoto hao wakati wakiwa ni wadogo. Loo, loo, ni jambo la aina gani!

89 Na jinsi gani watu wameketi huko, na kukiingiza kitu hiki ndani kwa sababu tu ya siasa! Vipi, sielewi mimi. Lakini sisi hapa, papa hapa kwenye asubuhi hii ya Pasaka. Na kitu kile kile, sababu yenyewe ya sisi kuja kwenye nchi hii, tukawa Wamarekani, ilikuwa ni uhuru wa dini dhidi ya mfumo huo wa Yezebeli, nasi tunageuka moja kwa moja na kuuchagua juu ya lile jukwaa huko juu katika Ikulu. Kitu kile kile ambacho tumekuja hapa tupate kuwa huru nacho! Loo, ni—ni hali ya ajabu sana ambayo tunaishi ndani yake sasa, mnajua hilo; kanisa la kiroho, kwa sababu limejiuza.

90 Walimwua, wakamwua kama tu walivyomfanyia Habili mwaminifu. Ni kwa nini Habili, akamwua. . .akauawa? Kwa sababu moyoni mwake alikuwa na ule ufunuo wa kukubalika na Mungu kile kilichohitajika kumkomboa mwanadamu kutoka dhambini. Hiyo ndiyo sababu yenyewe walimwua Yesu, kwa sababu ndani Yake mlikuwamo na ufunuo wa kile kilichohitajika kwa Mungu kuitibu dhambi. Hiyo ndiyo sababu hasa siku hizi wanalipinga Kanisa halisi la Mungu aliye hai, kwa sababu linahubiri tiba ya dhambi, mambo yanayowafanya watu waishi tofauti, watende tofauti.

91 Na wakati unapolishusha moja kwa moja ndani ya—ya kanisa tunaloishi ndani yake siku hizi, ukaliingiza kwenye makundi yetu ya Kipentekoste, wamerudi moja kwa moja huko nyuma, na kufanya jambo lile lile walilowekwa huru wasilifanye. Inaonyesha kuna kasoro mahali fulani. Tiba ya dhambi! Limeingia kwa urahisi sana, limenyemelea ndani kama tu, vema, kama tu chini ya udanganyifu wa kuficha ukweli halisi wa dini ya Kipentekoste. Lakini kama haitoi kitu cha namna hiyo, kama haitoi mazao ya namna hiyo, ina kasoro mahali fulani.

92 Boga linawezaje kuzaa tikitimaji? Haliwezi. Mzabibu unawezaje kuzaa mapichi? Hauyazai. Ukizaa mapichi, kuna

uhai wa mpichi ndani ya mzabibu.

93 Na hivyo ndivyo tujuavyo siku hizi. Endapo kanisa, haidhuru linakiri jinsi gani kuwa Kanisa la Mungu aliye hai, kama halimzai Mungu kwa wokovu wa zama za kale, kuwarejesha watu kwenye wokovu ha—halisi wa Mungu (na inaonyesha miongoni mwao, Mungu anaishi miongoni mwao), basi ni kitu kibaya, ni—hali—halizai Uhai ambao Kristo alisema lingezaa.

94 Kristo alikufa pale Kalvari. Jinsi ambavyo alipanda kwenye msalaba huo! Nilikuwa nikisoma kitabu kidogo hapa sio muda mrefu uliopita, ya kwamba katika namna fulani ya u—utafiti, na katika utafiti huu nilipata kitu cha kustaajabisha sana. Nikaketi chini, kisha nikakiweka hicho kitabu chini, nikainua mikono yangu na kumsifu Mungu, nikasimama na kuzunguka kidogo, kisha nikaketi chini na kukisoma tena. Nikawazia, "Loo, hivi hiyo ni kweli, kwamba juu ya kilima hiki hiki ambapo Yesu alisulubiwa, Adamu alikufa na kuzikwa katika kilima kile kile Yesu alipofia, na akazikwa kwenye kilima kile kile ambapo Adamu alifia; yeye alifia Golgotha, na akazikwa Golgotha?" Nikawazia, "Linafaa jinsi gani, liwe kweli ama si kweli."

95 Hebu tuseme ilikuwa ni kweli. Basi, Adamu wa kwanza alikufa na akazikwa, na yungali pale mavumbini, kwa sababu aliwakilisha ulimwengu na watu, kwa dhambi. Lakini Adamu wa Pili, akiwa ni Mungu wa Mbinguni, wakati alipokufa Golgotha, hapakuwapo na ardhi ya kutosha kumshikilia pale, Yeye alifufuka kwenye siku ya tatu na yu hai milele. Lakini shida ya dhambi ilitatuliwa!

96 Mungu aliitatua shida ya dhambi pale Kalvari, hapo ndipo deni ilipolipiwa. Wakati Adamu huyu, Adamu wa Pili, alipokufa, Yeye alilipa deni ya dhambi kwa ajili ya jamii ya binadamu.

Ndipo ulimwengu ukamlaza kaburini, na kumtia muhuri kwenye kaburi hilo.

97 Nao wangefanya jambo lile lile leo hii. Wanajaribu kufanya vile vile siku hizi. Sitaki mkose jambo hili. Ulimwengu unajaribu, nao utakuwa mbaya zaidi wakati wote, kumtia Kristo muhuri wamrudishe kaburini tena. Wanajaribu kumfanya Mungu wa kihistoria, Yule aliyetembea siku zile, na kuwapa nguvu wanafunzi kuwaponya wagonjwa, na kuwatoa pepo.

98 Lakini wao walifanya nini? Mara walipodhani wamemwondosha, kama tu vile Kaini alivyofanya wakati alipodhani alikuwa amemwangamiza Habili, walimtia muhuri kaburini, na kumwingiza mle ndani.

99 Na leo hii wanajaribu kumweka Kristo kaburini. Lakini, loo, yale asubuhi ya Pasaka iliyofanya! Asubuhi ya Pasaka iliharibu theolojia yao yote. Ndipo wakati asubuhi ya Pasaka ilipokuja kwa ajili ya watu, Kanisa hapa, miaka elfu moja mia tisa baadaye, nayo ikaiangamiza theolojia yao. Yeye hajafa, Yu hai milele! Hawawezi kumweka kaburini. Unaweza ukamweka

kwenye kaburi la Methodisti, ama kaburi la Baptisti, ama kaburi la Presbiteri, ama lolote unalotaka kufanya. Lakini Yeye—Yeye alifufuka kutoka kaburini, na yu hai leo! Nilikuwa na kaburi la Kibaptisti, nawe huenda ulikuwa na kaburi la Kimethodisti, lakini siku moja Yesu alifufuka kutoka kule, kutoka kuwa Mungu wa kihistoria, akawa Mungu aliye hai, aliyepo, aliye hai milele.

100 Jambo fulani lilitukia kwenye asubuhi hiyo ya Pasaka. Ilikuwa ni Muhuri, muhuri ulioidhinishwa. Walipomchukua wakamweka kaburini, na kutia muhuri wa Kirumi juu yake. Lakini wakati saa hiyo ilipowadia, wakati saa hiyo ilipofika! Yeye alikaa mle kwa kitambo kidogo, ni kweli, Yeye alikaa huko kwa siku hizo tatu usiku na mchana. Lakini kwenye wakati huo uliowekwa ambao Maandiko yalisema, Haleluya, kwenye wakati ambapo Yeye alisema, "Uharibuni mwili huu, na kwenye siku ya tatu nitaufufua"! Basi hakuna kitu kinachoweza kuyakomesha Maandiko hayo, hayana budi kutimia! Basi muhuri huo ukavunjwa, Naye akafufuka, Yesu yeye yule, yu hai tena milele!

101 Na kwa yapata miaka elfu moja mia tisa, ama labda nitasema miaka elfu moja mia nne ama elfu moja mia tano, makanisa yamemtia muhuri wakamweka mbali. Lakini Yeye alisema, "Itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu." Hakuna kitu kitakacholikomesha! "Itakuwa Nuru wakati wa jioni! Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya. Itakuwa Nuru wakati wa jioni!" Sijali ni mihuri mingapi mnayojaribu kuweka juu yake, Mungu atavunja kila muhuri. Aliuvunja ule muhuri wa kaburi. Aliuvunja muhuri wa kuzimu. Aliuvunja muhuri wa mauti. Aliuvunja muhuri wa kaburi, na kufufuka milele, akaishinda kaburi, mauti, kuzimu, makaburi, na kila kitu kilichobuniwa na wanadamu kilichokuwapo, kuonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu wala hawezi kutiwa muhuri atoke kwa watu tena. Mungu, milele! Hakuna kitu kinachoweza kumshikilia; kaburi lisingeweza kuchimbwa kwa kilindi cha kutosha, kuzimu isingekuwa na joto la kutosha. Loo, hakuna kitu kingaliweza kumshikilia! Yeye alivunja kila muhuri pamoja na Muhuri ule mkuu wa Krismasi, ama, si Muhuri wa Krismasi, bali Muhuri wa Pasaka aliokuwa ametiwa muhuri kwake. Na Yeye akasema, "Muhuri ule ule ninaovaa, nanyi mtauvaa pia, kwa kuwa . . . Nao muhuri huu nivaao, utafanya mambo yale yale wakati mmetiwa muhuri. Kwa kuwa yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya; hata kubwa kuliko hizi atazifanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba."

102 Utawezaje kuliweka chini? Utafanya nini, watu wanaweza kufanya nini kulihusu? Huenda . . . Umelazimishwa kwenye uamuzi, kufanya uamuzi wako utafanya nini kulihusu. Hiyo ni kweli kabisa.

103 Sasa, tunaona ya kwamba Yeye . . . hakuna muhuri

ungaliweza kumshikilia, Yeye alitoka. Mungu aliuvunja huo muhuri, muhuri wa kaburi, alivunja muhuri wa mauti, akavunja muhuri wa kuzimu, akavunja muhuri wa kaburi, na akatokea mshindi. Ni kitu gani kilichofanya hilo? Muhuri ule mkuu uliokuwa ndani Yake. Wangeweza kuuangamiza ule mwili, bali kamwe wasingeweza kuuangamiza Muhuri huo. Mungu alilipa Kanisa Muhuri, wakati huo, usioweza kuangamizwa. Wakati walipomwangamiza Habili, Yeye alimwinua Sethi. Walipomwangamiza nabii mmoja, kuliinuka mwingine. Waliendelea kuangamiza. Lakini Mungu akawapa kitu fulani, basi, ambacho hawawezi kuangamiza. Ni Roho wa kimbinguni; Ni Roho Mtakatifu Mwenyewe, wala Yeye hawezi kukosea wala kuangamia. Hawezi kuangamizwa. Ataendelea kuishi, na kuendelea, na kuendelea. Na kwa kuwa Yeye yu hai, sisi tunaishi pamoja na Yeye kwa kuwa tumetiwa muhuri katika Mwili wa Bwana Yesu Kristo. Hakuna njia, hakuna njia ya kuweza kuangamizwa, hatuwezi kuangamizwa, bali tuna Uzima wa Milele. Amina. Kurarua kukuu kwa Mungu kwa hiyo mihuri.

104 Pia alivunja muhuri mwingine ninaotaka kuzungumzia hapa, unaopatikana katika Kutoka. Ila sitakuwa na wakati wa kuyafungua Maandiko, bali Yeye . . . Yanayopatikana katika Kutoka. Wakati mwanadamu alipokuwa ametenda dhambi na kujitenga mwenyewe kutoka Uweponi mwa Mungu, naye akaja kumwabudu Mungu, kulikuwako na pazia lililoning'inia kati ya patakatifu na Patakatifu pa patakatifu. Ndani ya Patakatifu pa patakatifu kulikuwako na Utukufu wa Shekina. Hawakuruhusiwa kuingia Mle. Hawakuruhusiwa hata kupaangalia. Na mtu anayeingia mle, ilibidi apakwe mafuta mara moja kwa mwaka, avalie sawasawa, damu juu yake, damu mkononi mwake, damu kwenye bakuli, apate kukinyunyizia Kiti cha Rehema. Utukufu wa Shekina ulikuwa ni mkuu sana hata akapoteza fimbo mle ndani mwaka mmoja, akatoka bila (kuipata; akatoka) kuileta fimbo yake. Ndipo aliporudi, kitu hicho kilikuwa tayari kimekuwa hai, na kuchipusha, na kilikuwa na maua kila mahali, kwa sababu kilikuwa katika Uwepo wa Utukufu wa Shekina. Lakini kulikukwako na pazia lililoning'inia Pale katikati, kwa sababu kulikuwako na dhambi juu ya watu.

105 Lakini, loo, ndugu, wakati iliponyunyiziwa siku hiyo kwa Damu ya Yesu Kristo, Roho wa Mungu aliupasua huo muhuri kuanzia juu hadi chini, na kumrudisha mwanadamu. Sio tu kumweka mbali na Uwepo wa Mungu, bali Yeye alimrejesha kwenye Utukufu wa Shekina, akaingia katika Uwepo wa Mungu; ili yeye, maisha yake yaliyokufa . . .

106 Yesu alisema, "Ikiwa walifanya hivi katika mti mbichi, watafanya nini katika mkavu?" Na kama walimfanyia hivyo Yeye, akiwa ni Mti mbichi wenye Uhai, itakuwaje kwenye

maskini ule mti wa kawaida uliokufa usio na Uhai, mnaona, sasa wakati ghadhabu ya Mungu imemwagwa? Mti wa kale wa kawaida uliokufa unawezaje kustahimili hilo, wakati Mti mbichi, hata uliangamiza Mti mbichi, na kuutuma Wake, jehanamu? Ghadhabu ya Mungu imemwagwa kwa ajili ya kutokutii, kwa dhambi, ikaupeleka ule Mti mbichi jehanamu, itafanya nini katika mti mkavu wakati itakapoupiga? "Kama mwenye haki ataokoka kwa shida, mwenye dhambi na yule asiyemcha Mungu ataonekana wapi?" Huyo mtu anayeikataa ile Njia, huyo mtu anayejua vema zaidi, yule mtu ambaye imefunuliwa kwake, na angali anakataa kutembea katika Njia ya Mungu, itakuwaje kwa mtu huyo? Itakuwaje?

Naam, Yeye alivunja muhuri uliotutenganisha na Utukufu wa Shekina, kwa sababu dhambi ilikwisha sasa.

107 Na sasa muhuri ni ishara ya kazi iliyomalizika. Nasi tunajua ya kwamba muhuri, kama vile unavyoenda kutia behewa muhuri, vema, wanaingiza bidhaa zote ndani yake, na kuweka akiba kila kitu mle, kisha inatiwa muhuri hata kwenye kikomo chake. Muhuri wowote ni kazi iliyomalizika. Wakati unapoandika hati yoyote, basi inatiwa muhuri mwishoni. Haitiwi muhuri mpaka itakapomalizika.

108 Sasa, damu ya mbuzi na ya ndama, na kadhalika, isingeweza kuondoa dhambi. Lakini wakati hii ilipomalizika pale Kalvari, iliondoa dhambi. Sasa angalieni.

109 Kwenye bustani ya Edeni, kuwazuia watu wasirudi kwenye Mti huo, Mungu aliweka Malaika pale kama muhuri, akiwa na upanga uliozunguka pande zote, kuulinda Mti huo. Na wakati alipofanya ibada yake, naye akashuka. . .Sasa kumbukeni, ni Nani aliyekuwa kwenye Mti huo? Mti huo ulikuwa ni Nani? Ulikuwa ni Yesu.

110 Mti wa mauti ulikuwa ndio mama yako, yeye alikuleta hapa katika maisha ya kawaida. Kristo ni kule Kuzaliwa kupitia kwa Maisha ya Kiroho. Wote waishio kwa mwanamke, hufa; wote waliozaliwa na yule Mwanamume, huishi. Wote wanaokuja kupitia mwanamke, ni wa kawaida; wote wanaotokana na yule Mwanamume, ni wa Kiroho. Si huyu mtu *hapa*; Mwanadamu Kristo Yesu!

111 Basi angalia huo Mti, unalindwa; hauwezi kurudi, kwa sababu hakuna sadaka iliyowekwa kuondoa dhambi. Kwa hiyo basi walipokuja kuabudu, ule Utukufu wa Shekina ulikuwa nyuma ya pazia, umetiwa muhuri mbali nao. Ulitiwa muhuri wasiuone, tangu bustani ya Edeni.

112 Lakini hapo Siku ya Pentekoste ilipotimia, ndugu, wakati Yesu alipokufa pale Kalvari na kuimaliza hiyo kazi, Yeye hakumtia mwanadamu muhuri akamfungia nje, alimtia mwanadamu muhuri akamfungia ndani pamoja na Yeye Mwenyewe. Na sasa tumetiwa muhuri, na kufungiwa katika

Uwepo wa Utukufu wa Shekina. Sio kwamba tu tumetiwa muhuri ndani, bali tumetiwa muhuri Milele. Amina! Loo, napenda hilo, tumetiwa muhuri ndani sasa! Huo ndio Muhuri halisi wa Pasaka, "Kwa kuwa kwa Roho mmoja sote tumetiwa muhuri kuwa Mwili mmoja."

Mnasema, "Kwani Roho Mtakatifu ni Muhuri?"

113 Waefeso 4:30 ilisema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu ambaye kwaye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu." Huo ndio Muhuri halisi, wa kweli wa Pasaka. Unaonyesha ya kwamba dhambi imekwisha kulipiwa, kwa ajili yako, na Mungu amekukubali, nawe umetiwa muhuri katika Kristo kwa Roho Mtakatifu. Dhambi imekwisha. Muhuri wa Milele umemalizika.

114 Sasa tumefufuliwa leo hii. Ni kwa nini tunaweza kuwa na wakati kama huo juu ya mambo ya Mungu? Kwa sababu tumefufuliwa. "Wale aliowajua tangu zamani, Yeye aliwaita; wale aliowaita, Yeye aliwahesabia haki; wale aliowahesabia haki, Yeye amewatukuza." Basi sasa tumefufuka. Tumefufuka kutoka ndani kwenda nje, sio kutoka nje kwenda ndani. Loo! Hivi mnatambua? Sio kutiwa muhuri nje, *hivi*, bali kutiwa muhuri ndani. Loo, jamani, laiti kanisa lingaliweza tu kuliona! Mnaona, sisi hatujatiwa muhuri tukafungiwa nje, tumetiwa muhuri ndani. Hizo siku, wakati dhambi ilipokuwa—ilipokuwa ni chukizo mbele za Mungu, wala hapakuwapo na njia ya kuiondolea mbali, tulitiwa muhuri mbali nayo. Sasa wakati hiyo ilipopasuliwa vipande viwili, nao huo muhuri ukavunjwa na dhabihu ya dhambi iliyofanywa kutoka kwetu, sasa tumebatizwa ndani, na kutiwa muhuri ndani. Tumefufuliwa. Sasa tumefufuliwa, tayari tumefufuliwa. Unajuaje? Biblia ilisema hivyo! Amina. Sasa tumefufuliwa. Sasa tumefufuka pamoja na Yeye katika ufufuo wa kiroho. Neno *kuhuishwa* linamaanisha nini? *Kuhuishwa* kunamaanisha "ufufuo." Hiyo ni kweli. Tayari tumefufuka, sasa hivi, tumeketi pamoja katika Mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, tukiufurahia Muhuri wa Pasaka. Amina. Huo ndio Muhuri wa Pasaka ya kweli ya Mungu. Tuko namna gani? Kwa Roho mmoja tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, na kutiwa Muhuri Milele. Sasa tumefufuka, kiroho. Tulifufuka kutoka kwa kitu gani? Kutoka kwenye maisha ya dhambi, wakati mmoja tulikuwa wenye dhambi na tuliyapenda mambo ya ulimwengu.

115 Sasa, kuna watu wengi wanaosema ya kwamba wamefufuka, bali maisha yao yanathibitisha vinginevyo. Maisha yako yanathibitisha kile ulicho. "Kwa matunda yao mtawatambua," Yesu alisema. Hiyo ndiyo sababu kamwe tusingeweza kwenda juu ya kumfanya mtu anene kwa lugha na kusema yeye ana Roho Mtakatifu. Hatuamini hilo. Hakuna Maandiko kwa ajili ya jambo hilo. La, bwana. Watu hunena kwa lugha na kutoka nje na kuishi kama ulimwengu. Nao wanawake hunena kwa lugha na

wanakata nywele zao, wanajipodoa. Huh! Usingeweza kusema huyo alikukwa ni Roho Mtakatifu. Hakika siye, hasha, hasha. Mtu anavuta biri, naye anatoka hapa nje na kuishi na mke wa mtu mwingine, anatangatanga, anafanya vituko, ati useme huyo ni Roho Mtakatifu? La, la. "Kwa matunda yao mtawatambua. Mti mbaya hauwezi kuzaa matunda mazuri, wala mti mzuri kuzaa matunda mabaya."

116 Tumetiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu, Muhuri wa Pasaka ya kweli ya Mungu. Tumetiwa muhuri kuwa Mwili wa Kristo, tukatiwa Muhuri Milele. Sio muhuri kwa kipindi cha wakati; bali Milele. Na sasa mtu huyo ambaye ameupokea huo, amefufuka katika wafu, kutoka kwenye maisha ya dhambi. Ni kitu gani? Roho yake imefufuliwa, sha—shauku zake zimefufuliwa, maisha yake yamefufuliwa, yeye ni kiumbe kipya. Naye anakuja pamoja na wenyeji wenzake, kama tulivyo asubuhi ya leo, kuombeana, na kusaidiana, kuhimizana, na kuketi na kukusanyika katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, tumetiwa muhuri na Roho Mtakatifu. "Kwa kuwa mmekufa, na maisha yenu yamefichwa katika Kristo, kupitia kwa Mungu, yakatiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu," Maandiko yalisema. Hayo ni Maandiko. Sasa mnaona ya kwamba tumetiwa muhuri kwa Muhuri wa Pasaka. Muhuri wa Pasaka wa ufufuo, ambao ulithibitisha ya kwamba maisha Yake na yale aliyokuwa amesema yalikuwa ni kweli. Sasa tunaona ya kwamha ni kazi iliyokamilika, ni bidhaa iliyokamilika. Ufufuo wa Mungu ni bidhaa iliyokamilika. Roho Mtakatifu ni Muhuri wa Mungu wa bidhaa iliyokamilika.

117 Sasa tunamjia Kristo. Jambo la kwanza tunalofanya, tunahesabiwa haki kwa kumwamini Yeye. Tunapofanya hivyo, basi tunatambua ya kwamba tumefanya makosa, tunamwomba Mungu atutakase, hiyo ni kutusafisha kutoka maisha yetu ya dhambi. Martin Luther, kuhesabiwa haki, ujumbe wake. Kisha anakuja Wesley, pamoja na utakaso. Ndipo wakati yote yamekamilika, na Kanisa Lake limekamilika, ni nini kinachofuata? Kazi iliyomalizika. Kazi iliyomalizika ni Muhuri, kwamba Kanisa limekamilika.

118 Kama vile katika ile piramidi. Angalieni kwenye noti ya dola. Nimerejea kwenye hili. Sijui kama nimepata kulirejea hapa maskanini, au la. Mnaona katika noti ya dola, inaitwa "muhuri mkuu." Sasa ungewezaje kusema kwamba Marekani ingeweza kutambua ya kwamba huko Misri wao wana ule muhuri mkuu, nao huu hapa muhuri wa Marekani upande huo mwingine, tai? Kwa nini walazimishwe kuifanya hiyo muhuri mkuu, ule muhuri mkuu? Kwa sababu, kama ukiangalia, moja kwa moja nyuma, juu ya piramidi kuna bloku ndogo, na bloku hiyo ndogo ndiyo jiwe la kichwa, na jiwe hilo la kichwa kamwe halikuwekwa juu ya ile piramidi. Huko juu ni wazi, kama umewahi kuwa kule. Kwa neema ya Mungu, nimekuwako kule. Kwa hiyo hakuna—

hakuna kifuniko juu ya piramidi. Ni kitu gani? Henoko aliijenga kabla ya ile gharika. Ilikuwa ni ku—kumbukumbu, hiyo ndiyo sababu kamwe haikuangamizwa wakati wa ile gharika. Hakuna kitu kilichoiangamiza, kwa sababu ni kumbukumbu.

119 Sasa kama ukiangalia, huko chini kabisa ni pana, ndipo inaumbika juu kidogo zaidi katika uchache, kisha kidogo zaidi, ndipo inaingia kwenye lile jiwe la kichwa. Huo ni wakati wa Luther, kuhesabiwa haki katika Kanisa; kutakaswa; kisha ubatizo wa Roho Mtakatifu. Lakini inapoumbika kuelekea juu, inaendelea kutoka kwenye wakati wa Luther, hadi wakati wa Wesley, ikaingia kwenye wakati wa Kipentekoste. Lakini ikiisha kuuacha wakati wa Kipentekoste, inaendelea kuumbika mpaka inabidi kufikia mahali ambapo hata mawe hayo yote yamechongwa mpaka wembe. . .

120 Yana uzito wa tani na tani, huko juu. Jinsi walivyoweza kuyanyanyua huko juu, hiyo ingali ni fumbo kwa mwanadamu. Bali wanachukua wembe huu, nao wanaweza kuupitisha, nayo imechongoka kikamilifu sana hata huwezi hata kuweka wembe ambapo saruji inapaswa kuwa. Hivyo ndivyo hayo mawe yalivyowekwa pamoja kikamilifu. Na sasa wakati jiwe hili la kichwa, ambapo hayo mawe yameshikana namna *hii,* kidogo yamewekwa ndani, katika njia ya pembe ili kwamba lile jiwe la kichwa litakuja taratibu, na kuingizwa moja kwa moja ndani yake. Halitahitaji saruji yoyote, litakaa kikamilifu.

121 Sasa hivyo ndivyo Mungu anavyolifanyia kanisa Lake. Yeye anawachonga watu, na kulifanya kwa njia kamilifu sana, ili kwamba wakati lile Jiwe la Kichwa, Kristo, litakapokuja, linatoshea hilo jengo vizuri, ndipo ufufuo wa kitu hicho chote, Kanisa limenyakuliwa. Jiwe la Kichwa!

122 Sasa tumeketi pamoja katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu. Sasa tunatambua ya kwamba Yesu, ule mwili wa Yesu, ulitwaliwa juu kutoka kwenye ufufuo. Sasa tunajua ya kwamba Biblia inazungumza juu ya mbingu tatu. Tunajua hivyo, mbingu ya kwanza, mbingu ya pili, na mbingu ya tatu. Ninaamini ilikuwa ni Paulo ambaye alitwaliwa hata katika mbingu ya tatu na kuona mambo ambayo hayakumfaa yeye kunena habari zake. Sasa mbingu ya kwanza inaitwa, katika Maandiko, kama vile mawingu; kwa maneno mengine, huku chini, hapa kwenye muhuri wa duniani. Sasa wakati Anga hiyo kutoka huko juu ya mawingu inaposhuka kwenye Kanisa, hapo ni mahali pa Mbinguni. Halafu mbingu ya pili inahesabiwa ni mfumo wa jua. Nayo mbingu ya tatu inaenda mbele ya huo.

123 Sasa imetokea tu tumewazia, angalieni tu hili kwa dakika moja. Sasa, Einstein alithibitisha, kwa sayansi, ya kwamba kama vitu viwili vilikuwa vikikaribiana, kama vile magari mawili barabarani, na kama yalikuwa yakija upesi vya kutosha (sasa itayabidi kweli yawe yakienda kasi, kama maili bilioni

moja kwa sekunde) lakini yangeingiana moja kwa moja na yasisumbue kitu chochote. Hiyo kasi ingesababisha hilo, yaingiane pasipo kusumbua kitu chochote.

124 Sasa, sasa kama mtaangalia, nilikuwa nimesimama hapa sio muda mrefu kwenye Mlima Palomar, huko California, nami nilikuwa nikiona kule ile darubini inayoweza kuona maili milioni mia moja na ishirini ya uwazi wa nuru. Sasa wazieni, maili milioni mia moja na ishirini ya uwazi wa nuru, hizo zingekuwa ni maili ngapi kuhesabiwa. Mnaona?

125 Lakini hata hivyo Mbinguni ni maili bilioni na bilioni na bilioni kadha za—za miaka ya nuru kupita hiyo, mpaka hata haiwaziwi. Tungewezaje kufika Huko? Ni usafiri, itakukwa ni kama pamoja na nia, kasi sana, itakuwa kasi zaidi. Kama ungaliweza kuwazia juu ya Mbinguni, hivyo ndivyo upesi ungeweza kufika kule. Yesu, akiisha kufufuka, alikuja moja kwa moja kupitia kutani, moja kwa moja kupitia milangoni, na kusimama, na kula samaki aliyechemshwa, na sega. Haleluya. Kasi! Mara uhai ukiisha kutoka kwenye mwili huu, tuko Mbele za Mungu, huko ng'ambo. Tunajua tu mambo ya futi na inchi, na yadi na maili, na kadhalika, tuko kwenye mfumo huu usioweza kuondoka ardhini. Lakini tunapoondoka hapa, ndugu, loo, jamani, ni wakati wa jinsi gani!

126 Nikizungumza hivi majuzi usiku juu ya, Ibrahimu na Uzao wake baada yake, jinsi ambavyo Mungu alionyesha kupitia kwa Ibrahimu. Jinsi ambavyo alimhesabia Ibrahimu haki, mlango wa 12 wa Mwanzo. Na juu ya. . .huu na kuendelea, mlango wa 16, jinsi ambavyo alithibitisha lile agano kwa utakaso. Kwenye mlango wa 17, akamwacha ayanyonye matiti Yake, akavuta Roho Mtakatifu. Kisha akathibitisha, ama akamweka (kama vile mmenisikia nikihubiri lile somo la *Msikieni Yeye*), akamchukua Ibrahimu na kulibadilisha jina lake kutoka Abramu likawa Ibrahimu, akampa sehemu ya Jina Lake, Elohimu, h-i-m-u. Ndipo tunaona ya kwamba, baada ya hayo, Yeye alimtokea Ibrahimu.

127 Sasa kwa Uzao wake, angalieni vile alivyoufanyia ule Uzao vile vile. Uzao wa Ibrahimu ulipitia kwenye kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu; dhihirisho la Jina Lake, akifunua Yeye ni Nani (ufunuo huo wa Nani? Yesu Kristo), ubatizo katika Jina Lake, na kadhalika namna hiyo, ufunuo huo, akiligawanya Jina Lake pamoja na Kanisa Lake, akawaita watoke. Ndipo Yeye alifanya nini? Katika Kanisa lilo hilo ambalo aliliita kwa Jina Lake, Jina la Yesu, Yeye alifanya nini? Alionekana katika umbo lile lile alilomtokea Ibrahimu, akiweza kutambua roho nyuma Yake. Mnaona? Alionekana katika Jina lilo hilo, katika kitu hicho hicho, katika umbo lile lile! Tuko tu katika mwisho wa safari.

128 Sasa angalia kile kilichotukia. Wakati alipofanya hivyo, hiyo

ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho aliyolipa Kanisa kabla badiliko halijaja Kanisani, kwa Ibrahimu na Sara. Sasa wakati yule Malaika alipofunua ile siri, yule mwanamke (Kanisa, ambalo aliwakilisha), ilikuwa ni vigumu kwake kuliamini, alicheka tu moyoni mwake. Mnaona, yeye alikuwa na umri wa miaka mia moja, yeye na Ibrahimu walishindwa kuwa kama mume na mke. Mnaelewa yale ninayomaanisha, uhusiano wa kifamilia, labda miaka ishirini hapo kabla; vema, walikuwa wamekufa kwa njia hiyo. Sara; Ibrahimu kama mtu aliyekufa, tumbo la uzazi la Sara ni kama limekufa. Lakini ni kitu gani kilichotukia? Ni kitu gani kilichofanyika? Akasema, "Ningewezaje, nikiwa mkongwe jinsi nilivyo, naye bwana wangu, hatujaninii . . . tumekoma njia hiyo, tumekoma njia hiyo kwa muda wa miaka mingi, mingi sana. Haiwezekani kwake. Haiwezekani kwangu. Ninawezaje kufanya hivyo?" Ndipo akacheka moyoni mwake.

129 Naye Malaika akasema, "Kwa nini akacheka? Kwa nini akawazia moyoni mwake? Kwa nini akasema hivi?" Sasa angalieni, hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho kabla jambo fulani halijatukia kwa Sara na Ibrahimu.

130 Sasa nilihubiri hapa wakati mmoja, na kuwaambia ya kwamba Mungu aliwageuza wakawa kijana mwanamume na mwanamke. Kulithibitisha, alishuka, walifanya ziara ndogo wakashuka kwenda Ge—Gerari, naye Abimeleki, yule mfalme wa Kifilisti, akampenda Sara, naye alitaka kumwoa. Hakika, alikuwa msichana tena, mrembo. Pia angalia, ilimbidi Yeye kufanya jambo fulani, ilimbidi kumbadilisha. Yeye hakumrudisha tu kuwa kijana mwanamume na mwanamke, huyo mwanamume na mwanamke, Yeye hakufanya hivyo; kwa sababu, kama wangerudi hivyo, jambo lile lile lingeendelea kuwako. Mnaona, wangekuja moja kwa moja . . . kwa kuwa yeye alimwoa alipokuwa na umri wa yapata miaka kumi na sita, naye alikuwa tu ni kijana mwanamume, nao waliishi maisha yao yote bila watoto. Kama Yeye angaliwarejesha tu nyuma, vema, wangalifanya tu jambo lile lile tena. Lakini ilimbidi kufanya jambo fulani tofauti, ilimbidi kuwabadilisha kusudi waweze kumpata huyu mwana aliyeahidiwa, yule mwana aliyeahidiwa waliyekuwa wanaenda kumpokea. Lakini ilimbidi kubadilisha mfumo wao wote, na kuwarejesha kuwa wachanga *na* kuwabadilisha, wapate kumpokea huyo mwana.

131 Jambo lile lile atakalofanya tena! Baada ya hilo, kumbukeni, baada ya ishara hiyo kudhihirishwa kikamilifu kwa Ibrahimu na kundi lake, basi jambo lililofuata lilikuwa ni kubadilishwa huko. Mnaona? Sasa tayari tumeona kila kitu kupitia kwa kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, kuwekwa kwa mwana, na ishara na maajabu Yake, kuwa katika Uwepo Wake ili kuyatambua mawazo ya moyo, na kadhalika, kama Yeye alivyosema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Tunaona

hilo likitukia sasa hivi! Jambo la pili lilikuwa ni nini? Kule kubadilishwa kwa mwili. Sasa, kuonyesha ya kwamba hili ndilo tunalotazamia, Mwana anayetarajiwa. Utukufu! Hiyo ni kweli? Hatuwezi kukutana na Yeye katika miili hii. Kama tukibadilishwa kuwa vijana wanaume na wanawake, bado hatuwezi kumlaki Yeye, kwa sababu inatubidi kumlaki hewani. Hapana budi jambo fulani lifanyike mbali na kutubadilisha kuwa vijana wanaume na wanawake, hatuna budi kubadilishwa na kutwaliwa juu hewani kumlaki Yeye. Nalo jambo linalofuata ni kule Kunyakuliwa kwa Kanisa, na kubadilishwa kwa mwili wa watakatifu waliolala mauti, kumlaki Bwana Yesu hewani.

132 Loo, kumbukumbu ya Pasaka, wale ambao wametiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu! Sasa kwenye lango la Edeni, mwanadamu alitiwa Muhuri atoke kwa Mungu, pale Pentekoste yeye alitiwa Muhuri Milele ndani ya Mungu. Yeye haingii wala kutoka tena, yuko Huko milele! Angalieni! Roho mmoja, "Tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, kwa Roho Mtakatifu." Hiyo ni kweli? Ndipo tumetiwa muhuri hata muda gani? Hata siku ya ukombozi wenu! Hatoki tena kuyaendea mambo ya ulimwengu. "Kwa kuwa mmekufa, na maisha yenu yamefichwa katika Mungu kupitia Kristo, mkatiwa Muhuri ndani kwa Roho Mtakatifu." Loo, ni Andiko zuri jinsi gani, kutiwa muhuri ndani ya Kristo kwa Roho Mtakatifu!

133 Ndipo wakati Yesu alipofufuka katika wafu, mwanadamu alilazimika tena kufanya uamuzi wao, "Hivi Yeye alifufuka, ama hakufufuka?" Nao walifanya nini? Walifanya jambo lile lile walilofanya kwenye ile kesi ya dhihaka, siasa na kanisa pamoja; kwa maana siasa na dini ziliungana pamoja kama vile zilivyofanya wakati huo.

134 Kama tu vile zitakavyofanya siku za usoni, na wanavyofanya sasa hivi, siasa na dini! Ahabu alikuwa ni jamaa mzuri sana, bali Yezebeli, yeye alikuwa amemwoa. Sisemi ya kwamba Rais Kennedy si mtu mzuri, bali ameolewa na mfumo huo wa Yezebeli. Si Ahabu aliyefanya hilo, ilikuwa ni Yezebeli nyuma ya kile kiti cha enzi, aliyeliongoza. Ni ule mfumo wa Yezebeli utakaosababisha uharibifu hapa. Hana budi kufanya hivyo, maana amemwoa. Hana budi kulipokea, hana budi kufanya hivyo, yeye amemwoa. Loo, jamani! Enyi watu, hivi hamwezi kuona yale Maandiko yanayofanya? Hivi hamwezi kuona mahali tunaposimama hapa katika siku za mwisho?

135 Sasa angalieni mtu baada ya ufufuo. Mmeona kesi hiyo ya dhihaka, wakaigeuza kwa kanisa, wakijua yale kanisa lingefanya. Basi ilikuwaje wakati askari hawa walipoogopa na kukimbia? Kanisa liliwakodi askari hawa, nao wakapewa pesa, waende wakaseme ya kwamba "Wanafunzi Wake walikuja usiku wakamchukua."

136 Basi nataka kuwaulizeni. Ikiwa wanafunzi walikuja usiku

wakamchukua, kwa nini hawakulichukua lile joho alilokuwa amevaa? Kama walikuwa ni wezi, na wanaiba, kwa nini hawakulichukua hilo joho, pia? Lakini hiyo kitani ilikuwa imewekwa pale pale, na kile kitambaa juu ya uso Wake, kitani imewekwa mahali ilipokuwa juu ya mwili Wake. Yeye aliondoka moja kwa moja kupitia yote hayo, akapanda juu kufikia ufufuo. Hakuna kitu kilichovurugwa; jinsi tu alivyokuwa amelala, Yeye alikuwa amelala jinsi ile ile, bali alikuwa ametoka kwenye hiyo kitani. Amina.

137 Mnaona, ila ni kesi ya dhihaka tena, sh—sh—shtaka la uongo. Kwa sababu gani? Walilazamishwa, walilazimishwa kufanya uamuzi. Ilimbidi mwanadamu kufanya uamuzi. Ilibidi kanisa liseme, "Amefufuka katika wafu," ama "Hajafufuka katika wafu." Amina.

138 Loo, hebu tuuchukue usikivu wetu sasa, vaeni vyombo vyenu vya kiroho vya kusikizia. Angalieni, imefika kwenye jambo lile lile. Watu wanajaribu kufuata, kama vile mikutano yetu, na kusema . . . Nimesikia hata makanisa, Kanisa la Kristo, linavyojiita, kasema, "Nitatoa dola elfu moja kwa mtu yeyote anayeweza kuonyesha thibitisho la ufufu- . . . ama mtu ambaye ameponywa." Nimewapeleka madaktari kwao, wala hata hawangeamini. Kwa nini? Wamelazimika kufanya uamuzi. Wamejitia muhuri nje, pamoja na Kaini, pamoja na makundi ya dini potovu. Kanisa dogo la kweli la Mungu liko katika uchache, bali sikuzote lilienda hivyo, bali litaninii . . . Lilistahimilije miaka hiyo elfu moja mia tano ya nyakati za giza?

139 Wao husema, "Kanisa la Kirumi!" Hakika, kanisa la Kirumi kwanza lilikuwa kanisa la kipentekoste, kanisa Katoliki lilikuwa hivyo. Lilianzia pale Pentekoste, lakini basi lilitaka kujiundia dhehebu.

140 Na kama kanisa hili la Kipentekoste lingesimama kwa miaka mingine elfu mbili, wangekukwa wabaya kuliko Katoliki ilivyo sasa. Wanaenda mbali sana na kila kitu! Niliulizwa swali hivi majuzi, "Hivi utahubiri kama ukija mahali hapa, juu ya wanawake kujipodoa, hawapaswi kuvaa kaptura, hawapaswi kuvaa vitu hivi?"

Nikasema, "Msinialike basi. La, bwana. Msinialike kuja."

"Utahubiri hivyo?" Hata walisema, "Una shughuli gani na hilo?"

Nikasema, "Ni kazi ya Bwana, nami ninafanya kazi Yake." Hiyo ni kweli kabisa. Kabisa! Kwa hiyo nikasema tu . . .

"Unafanya hilo kwa sababu gani? Kwani si kuna mambo mengine ya kusema?"

Nikasema, "Naam, lakini hebu wafanye hivyo, ndipo tutazungumza juu ya mambo mengine, mnaona. Mnaona? Mnaona, hebu—hebu—hebu na tuweke msingi."

141 Hiyo ndiyo shida yake. Mnajaribu kuruka juu ya ngazi, wakati mnapaswa kuwa huko chini bado. Mnaona? Anzieni *hapa* chini, fagieni na muanze vizuri, ndipo tunaweza kujenga juu ya huo. La sivyo, huwezi kujenga, kwa sababu msingi wowote ambao haujajengwa juu ya kanuni za Kristo utaanguka. Nayo Biblia, ilisema, "Ni chukizo kwa mwanamke kuvaa mavazi yampasayo mwanamume." Halijabadilika hata kidogo kwa kuwa Mungu hajabadilika. Yeye ni wa Milele, nayo mawazo Yake jana ni kama yalivyo leo, na yatakavyokuwa milele. Roho Wake ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kazi Zake ni zile zile jana, leo, na hata milele. Ukombozi Wake ni ule ule jana, leo, na hata milele. Na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Hakuna njia ya kulikwepa. Sasa thibitisho la pudini ni kuila. Tunajua hilo. Hiyo ni kweli? Mungu alisema ilikuwa hivyo.

142 Mwanadamu alilazimika kufanya uamuzi. Ni kitu gani walicholazimishiwa kwanza katika siku za Kristo? Walilazimika kufanya nini? Walilazimika, kwanza, kumkubali Yeye. Yeye aliwaonyesha ishara Yake, Muhuri Wake, Yeye alikuwa ni Masihi! Yeye alilionyeshaje? Kwa yale hasa Biblia iliyosema angefanya. Yeye alikuwa ni Nabii, Naye akayatambua mawazo niani mwao. Nao wakasema, "Yeye ni ibilisi, Beelizebuli." Walilazimika kufanya uamuzi. Wasingeweza kuushikilia tena.

143 Wala na kanisa la Kipentekoste, ama la Kibaptisti, ama la Kipresbiteri! Roho Mtakatifu ameninii . . . Kristo amefufuka, na Yeye yuko Kanisani. Nao wanasema, "Mtu huyu hubatiza katika Jina la Yesu. Anaamini haikubidi kunena kwa lugha kwa ajili ya Roho Mtakatifu, na mambo kama hayo, ya kwamba huo sio ushuhuda wa kwanza. Anaamini katika wanawake, wanawake wetu wote kuziweka nywele zao jinsi hiyo. Nafikiri halina uhusiano nalo." Basi ni kwa nini Mungu anathibitisha ya kwamba Hii ni Kweli? Tafuta mahali ilipo.

Waliukataa Umasihi Wake wakati Yeye alipowaonyesha Yeye alikuwa Masihi. Walilazimika kusema jambo fulani.

144 Na ndivyo walivyo siku hizi, kulikataa, wala wasingelidhamini, huku wakinawa mikono yao kutoka Kwalo. Wanalazimishiwa uamuzi. Hakuna njia ya katikati! Tuko kwenye wakati wa mwisho. Mwanadamu analazimika kulipokea ama kulikataa. Inakubidi kulipokea ama kulikataa. Limelazimishiwa Marekani. Limelazimishiwa Maskani ya Branham. Limelazimishiwa Wapentekoste, juu ya Wamethodisti. Limelazimishwa kila mahali. Inakubidi kulichukua ama kuliacha. Mungu amelithibitisha Neno Lake, akionyesha ishara Zake, akiiunga mkono huduma Yake, akionyesha hasa kile Yeye alicho, kwa kuthibitisha ya kwamba Yeye ni Mungu. Yesu alisema, "Nisipozifanya kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi." Hiyo ni kweli. "Lakini kama nikizifanya kazi za Baba, basi amininі hizo kazi." Haya basi. Mnaona, hawawezi, wao—wao—wao hawawezi kupata kitu kwenye Hilo, kwa sababu

Hilo ni kweli. Basi ni kwa nini wasilipokee? Ni kwa sababu ya dhehebu. Hawawezi kulipokea, kwa hiyo wanalazimika sasa kufanya shindano la kuamua.

145 Na huko Ohio siku chache tu zilizopita, makanisa yale yale yaliyonidhamini mwaka mmoja uliopita; kwa sababu nililishambulia, na kuonyesha kwamba ilikuwa ni makosa, hapakuwapo na moja la hayo, ila kanisa moja, Ndugu Sullivan, lingeshiriki. Nikasema, "Ningali nina mkono ule ule, ningali nina miguu ile ile, ningali nina Ujumbe ule ule, ningali ni Ndugu Branham. Nina shida gani?" Sio mimi. Roho Mtakatifu angali ananena, Roho Mtakatifu angali anafanya kazi zile zile, angali anazionyesha. Lakini unalazimika! Hiyo ni kweli, wanalazimika. Naye yule Roho Mtakatifu mkuu akishuka moja kwa moja miongoni mwao, na kuzungumza Maneno na kusema mambo ambayo Yeye aliyasema wakati huo. Ndipo wangali . . .

146 Angalieni hapa California hivi majuzi. Ninafikiri ninaweza kulipata hapa; hili hapa. Nilikuwa katika Mkahawa wa Clifton, kwenye kiamshakinywa. Na hapo ndugu wa Kibaptisti . . . baada ya mimi kumalizia kuyararua makanisa vipande-vipande, kuwaambia jinsi walivyokuwa wakifanya maovu, na mambo waliyokuwa wakifanya, kumkataa Mungu. Ndugu huyu wa Kibaptisti akaja hapa kuniwekea mikono, kuomba. Basi, alipofanya hivyo, alianza kunena kama katika lugha. Wakati yeye . . . Sasa, yeye alikuwa ni Mbaptisti, hakujua lolote kuzihusu. Wakati alipomaliza, akasema . . .

147 Naye mwanamke aliyesimama kule nyuma, kutoka Louisiana, Mfaransa, akasema, "Hiyo haikuwa ni lugha isiyojulikana, hiyo ilikuwa ni Kifaransa,." Kisha hapa aliketi mwanamke mwingine kutoka Uswisi, Lausanne, ambaye anazungumza Kifaransa, (Nimekuwa kule), akasema ya kwamba aliitafsiri vizuri. Huyu hapa akaja kijana mwanamume akitembea kule chini (Sijawahi kumwona, hakuna mtu aliyekuwa amewahi kumwona), alikuwa ni mfasiri wa Kifaransa wa U.N., kasema, "Kweli kabisa, ni sahihi," kasema.

148 Naye mtu huyu anasema, nanyi mnamjua mtu huyu, nitalitaja jina lake katika dakika moja. Jina lake lilikuwa ni Henry. Nitalipata jina lake la mwisho katika dakika moja, nafikiri limeandikwa hapa. Sijui. Liko kwenye Sauti ya Wafanyabiashara, kama haliko. Lakini yeye . . . Loo, naam, "Na Danny Henry." Sasa hiyo ni . . . Siwezi kumkumbuka huyo bingwa wa sinema. [Mtu fulani anasema, "Marilyn Monroe?"—Mh.] La, si Marilyn. Meda, alikuwa . . . ? Jane Russell, binamu wa Jane Russell. Ndipo akapanda juu na kunikumbatia kwa mikono yake, kunipongeza, nayo haya hapa maneno aliyosema. Yeye alisema, "Mahubiri hayo yangewekwa katika Kitabu cha Ufunuo." Kasema, "Ni kweli." Akasema, "Ninataka kukuombea, Ndugu Branham." Akanikumbatia kwa mikono yake, akaanza kunena katika Kifaransa, wala sikujua lolote kulihusu.

149 Basi hii hapa ilikuwa ndiyo tafsiri, ameiandika jinsi makala yanavyotolewa, katika muundo, na kadhalika. Yalisema, "Mimi, Victor D-e D-o-w-x," jina la Kifaransa, "mimi ni Mfaransa," na kadhalika, "nami nilikuwako wakati—wakati Danny" *unalitamkaje*, "Danny Henry, alipotoa huu katika ujumbe juu ya Ndugu Branham, tarehe kumi na moja Februari, 1961." Yeye anaishi kwenye Barabara ya Kings 809, Los Angeles 64. Sikilizeni—sikilizeni ikisomwa:

> *Kwa sababu wewe umechagua njia nyembamba . . .*

Sasa, mnaona, ninalipata hilo lote vizuri. Kuna sehemu yake sijui.

> *Kwa sababu wewe umechagua njia nyembamba, njia ngumu, umetembea kwa chaguo lako mwenyewe . . .*

150 Ninaweza kulipata hilo vizuri, mnaona. Mnaona, unajichagulia mwenyewe. Musa alifanya chaguo lake mwenyewe, haikumbidi kufanya hivyo. Wala haikunilazimu kupitia njia hii. Ningalikuwa na majengo makubwa huko nje kama baadhi yao walivyo nayo. Ningeweza kuwa kila mahali katika televisheni. Lakini nani angenidhamini huku—huku nikishambulia ule msingi wenyewe? Lakini jambo moja, hainibidi kuinama miguuni pa mtu yeyote ila Bwana Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Naam. Ninahubiri yale Biblia isemayo. Hainilazimu kupatana na madhehebu yao, maana mimi si mfuasi wa hayo. Nilifanya chaguo. Kama tu vile Yeye alivyosema huko juu, "Kama nlivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja nawe." Naye alimpa Musa ishara mbili za thibitisho, kuthibitisha. Naye Musa akafanya chaguo lake mwenyewe. Mnaona, Musa alifanya chaguo lake mwenyewe. Kwa hiyo hilo ni rahisi kuelewa hilo, mnaona, "Umechagua . . . "

> *Kwa sababu wewe umechagua njia nyembamba, njia ngumu, umetembea kwa chaguo lako mwenyewe . . .*

Sasa hapa, sasa mtu huyu, sasa angalieni jinsi ilivyoandikwa, mnaweza kuona imeandikwa katika—katika maneno ya kigeni.

> *. . . wewe umechagua uamuzi mzuri na sahihi, nayo ni NJIA YANGU.*

Abarikiwe Mungu! "Ni *NJIA YANGU*," Yeye alisema.

> *Kwa sababu ya uamuzi huu muhimu sana, sehemu kubwa sana ya Mbingu inakungojea.*

Yeye hakuwa amesikia kuhusu lile ono, mnaona, la hili, mnalikumbuka lile ono.

> *. . . sehemu kubwa sana ya Mbingu inakungojea. Ni uamuzi adhimu jinsi gani ulioufanya!* (Mnaona?)
>
> *Hili, lenyewe . . .*

Sasa hapa ndipo, tangu hapa na kuendelea, sielewi.

*Hili, lenyewe, ndilo* (Limezungushiwa mabano makubwa.) *ambalo litatoa na kutimiza ule ushindi mkuu sana katika Upendo wa Kiungu.*

151 Sijui hilo linamaanisha nini, “hili litafanya litimie.” Labda kwenye lile hema dogo moja ya siku hizi, nikiketi huko nyuma, Yeye atafanya lijulikane.

152 Kwa nini? Si kwa sababu ilitubidi kufanya hivyo. Si kwa sababu kwamba—kwamba ni—ni—ni njia rahisi tu. Unaweza kuwa maarufu, ungekuwa na kila mtu akikupapasa mgongoni, pesa zikiingia kutoka kila mahali kwa ajili ya redio ama televisheni, na kadhalika. Wao walisema wangeuchukua na kuuweka kwenye televisheni. Siamini katika kuvichukua vitu vya Mungu na kuviweka huko nje kwenye upuuzi kama huo wa kishenzi wa ulimwengu. Siamini katika makelele haya yote na kufanya kitu ambacho hakipo. Ninaamini katika kuliacha tu, kungojea. Mungu, Yeye ni Mungu, acha afanye nalo yale atakayo kufanya. Sisi ni watumishi, tumtumikie tu Bwana, tufanye tu kama Mungu alivyosema. Mwanadamu, katikati ya yote hayo, hata hivyo, analazimika kufanya uamuzi.

153 Walilazimika kufanya uamuzi wakati Kristo alipokuwa hapa duniani, kwa sababu Yeye aliwathibitishia alikuwa ni Masihi. Hiyo ni kweli? Nao walilazimika, nao wakamwita nini? “Beelizebuli, mpiga ramli.” Ndipo ninii Yake. . .kwa ishara Yake, Muhuri, kwenye Pasaka, Mungu alilithibitisha, ya kwamba Yeye alimfufua katika wafu. Baada ya mambo haya mengine yote, Yeye alimfufua katika wafu!

154 Sasa kanisa linalodai kuwa na Roho Mtakatifu, thibitisho lake la Mungu, ya kwamba umepita kutoka mautini kuingia Uzimani, kwa sababu mambo ya kale yamepita, na mambo yamekuwa mapya kwako. Hilo ndilo thibitisho la Mungu la ufufuo. Huko jinsi ulivyokuwa, umebadilishwa! Ambapo ulikuwa ukitilia shaka Neno la Mungu; kila Neno Neno la Mungu lisemalo, unasema, “Amina!” Unaona, kuna jambo fulani lililokupata. Huo ni mfano wa kwanza tu wa ufufuo, Roho akiwa ndani.

155 Sasa Pentekoste. Baada ya Pentekoste, wakati watu hawa walipompokea Roho Mtakatifu, mwanadamu alilazimika tena kufanya uamuzi, “Hilo ni la Mungu ama si la Mungu?” Nao walisema nini? “Hao ni wazushi. Hicho ni kichaa. Wamedanganyika.” Hata Agrippa alimwambia Paulo, “Una wazimu.” *Wazimu* linamaanisha “kichaa.”

156 Basi Paulo alisema nini? “Katika njia iitwayo uzushi, hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu.” Yeye alikuwa na Muhuri wa Pasaka! Alikuwa kule wakati jambo fulani lilipotukia. Nina furaha kushikana mikono naye asubuhi ya leo, moyoni, na kusema, “Paulo!” Kwa nini? Ingetulazimu kuhubiri Neno lile lile. Paulo aliwaamuru kubatizwa tena, katika Jina la Yesu,

baada ya wao kubatizwa vinginevyo. Akasema, "Kama malaika kutoka Mbinguni akisema jambo lingine lolote, na alaaniwe." Yeye alihubiri Uponyaji wa Kiungu. Alihubiri nguvu za ufufuo. Alihubiri Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Maono, na nguvu na madhihirisho ya Roho yalimfuata.

157 Itakubidi kuwa na Ujumbe ule ule, jambo lile lile. Sio thiolojia, sio matendo fulani ya kanisa; bali Nguvu za Mungu, Pentekoste, na Muhuri ule ule. Muhuri wa Roho Mtakatifu, Muhuri wa kweli wa Pasaka ya Mungu ndio utambulisho wa mwanadamu. Kweli! Ni haki yako ya mzaliwa wa kwanza. Ni utambulisho ya kwamba umepita kutoka mautini kuingia Uzimani, naye Mungu anatenda kazi kupitia kwako kama vile alivyofanya Bwana Yesu, kwa sababu ndio utambulisho wako. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Enendeni ulimwenguni kote," baada ya Pasaka, baada ya Pentekoste, baada ya Muhuri wa Pasaka kutolewa, wa ufufuo. Ilikuwa ni kitu gani? Uhai uliokuwamo ndani ya Kristo uliofufuliwa, umekuja na kulihuisha Kanisa Lake, na unaishi Kanisani kufanya ishara zile zile.

158 Ninatumaini halitapitia juu ya kichwa chako. Ninatumaini siwaweki kwa muda mrefu sana hata ha—hamta—hamtapata furaha ya yale ninayomaanisha, mnaona. Ninajua ni vigumu, ninyi watu mnaosimama. Tafadhalini, dakika cha—chache tu, jaribuni mkiweza. Mnaona, ninataka uipate hoja hii, rafiki. Ninataka uone kile kilicho moyoni mwangu, kile kimekuwa hapa miaka thelathini na mmoja, tangu nilipoliweka maskini jiwe lile la pembeni hapa pembeni. Mnaona, kunayo Kweli, nimejaribu kuitetea. Kumekuwako na kila namna ya mambo yaliyotokana Nayo, ambayo ni ya kweli, lakini daima imekuwa hivyo.

159 Nilikuwa nikisoma juu ya Martin Luther, kasema, "Ilikuwa ni vigumu kuamini ya kwamba angeweza kupinga kanisa Katoliki na kuepuka. Hilo lilikuwa ni jambo kuu. Lakini jambo kubwa kuliko yote, ni jinsi angeweza kukishikilia kichwa chake kwa utulivu juu ya ulokole wote uliofuatana na uamsho wake, hata angeweza kudumu mwaminifu katika Biblia." Sema yale Mungu asemayo, na usiseme jambo lolote lingine. Dumu tu moja kwa moja na Hilo, tembea katika uamuzi wa moja kwa moja, sahihi wa Mungu. Badala yake. . .Kama Mungu akiamua liwe *hivi*, hebu tukae moja kwa moja Nalo. Huo ndio uamuzi Wake. Amina. Naam, bwana. Naam, bwana.

160 Mu—Muhuri wa Pentekoste ndio utambulisho wa mwaminio kwamba amepita mautini kuingia Uzimani, kwa kuwa amepokea Baraka za pentekoste, Muhuri wa Pasaka ya Mungu kwa Mwana Wake. Yeye alimtia muhuri Mwana Wake wa kwanza kwa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli? Kweli. Naye aliwatia muhuri watoto Wake wengine wote kwa Roho Mtakatifu.

161 Sasa tunaona hapa ya kwamba katika kutia muhuri hili sasa

kwenye wakati huu, kwa kuwa wakati wa mwisho unakaribia. Kuna mahali hapa ninapopaswa kupafikia, kuhusu wale wana, wana wa Kaini huko nje sasa, wamelazimika kufikia mahali ambapo hawana budi kufanya uamuzi. Mnaona, ni vigumu kwao kufanya, kwa sababu, wakifanya, inawabidi kupoteza haki zao za kimadhehebu. Mnaona? Ndivyo pia ilivyokuwa na Mafarisayo. Mnajua, Mafarisayo walifanya uamuzi juu ya Yesu, wakati alipothibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi. Basi wakati Roho Mtakatifu ameithibitisha Njia hii inayoitwa uzushi, ambayo imethibitishwa kwamba ni Roho Mtakatifu, mwanadamu hana budi kufanya uamuzi. Hawawezi kusimama kimya.

162 Hapa hivi majuzi usiku, nilikuwa nje, nikimwombea mwanamke mgonjwa hospitalini. Ndipo niliposhuka, nilimsikia mtu fulani akipaza sauti, "Billy!" Nami nikaangalia kote. Ilikuwa ni mmoja wa ndugu zetu hapa, yeye huja hapa, Roy Slaughter. Alikuwa amesimama huko chini ukumbini kutoka kwangu, mbali kidogo, naye akasema, "Mke wa ndugu yangu ni mgonjwa. Hivi utaingia na kumwombea, Billy?"

Nami nikasema, "Hakika."

163 Nikaingia mle ndani. Na kulikuwako na mama mwingine mkongwe, yapata umri wa miaka sitini, amelala pale, ilionekana kana kwamba mwanaye alikuwa ameketi karibu naye. Baada ya kuzungumza nao kidogo, nikasema, "Twaweza . . . Tutaomba."

Akasema, "Funga hilo pazia!"

Nami nikasema, "Vema." Nikasema, "Wewe ni mwaminio?"

Akasema, "Mimi ni Mmethodisti."

Nikasema, "Hilo silo nililokuuliza." Nikasema, "Wewe ni mwaminio?"

Akasema, "Mimi ni Mmethodisti. Sisi ni Methodisti. Funga tu hilo pazia!"

164 Sikulifunga. Niliomba, kwa vyovyote vile, na kumwombea, kwa hiyo niliomba Mungu amwokoe. Lakini jambo ndilo hilo, mnaona, wewe si Mkristo, wewe ni Mmethodisti. Unaona, wewe—wewe si mwaminio, wewe ni Mmethodisti. Ushuhuda wako mwenyewe unalielezea. Aturehemu, jamani, ni umbali gani unaoweza kuanguka kutoka kwenye Biblia?

Waaminio! "Na ishara hizi zitafuatana ha hao waaminio!"

165 Wewe ni Mkristo? "Mimi ni Mmethodisti." Hiyo inaonyesha wewe si Mkristo. Wewe ni Mkristo?' "Mimi ni wa Church of Christ." Hiyo inaonyesha ya kwamba wewe si Mkristo.

166 Wewe ni Mkristo kwa sababu wewe ni mwaminio. Na kama wewe ni mwaminio, Yesu alisema katika Marko, mlango wa 16, "Ishara hizi zitafuatana na hao waliopokea Muhuri wa Pasaka, hata ukamilifu wa dahari." Hiyo ni kweli, wewe ni mwaminio.

167 Nao watu wanalazimika, wanalazimika sasa. Kitu hicho kinafanya kazi, nao wanalazimika kukipokea ama kukilaani. Nao wanafanya nini? Kukilaani.

168 Lakini asingefanya hivyo kule nyuma kwenye ule wakati wa Pentekoste, kwa sababu Pentekoste inarudi nyuma moja kwa moja na kuunda dhehebu, inakuja, wakijiundia dhehebu wakawa kitu kile kile ambacho ndio kwanza wajiondoe kwacho. Pentekoste ilitoka. Pentekoste si dhehebu, pentekoste ni tukio linalompata mwaminio. Lakini walifanya dhehebu kutoka kwake, nao wamefanya jambo lile lile walilopigania sana kutoka kwake.

169 Jambo lile lile taifa na siasa zilifanya, wakaja huku kwa ajili ya uhuru wa dini, kutoka kwenye maskini fundisho la kikahaba la Katoliki; nao wakarudi moja kwa moja na, kwa upofu wa siasa, wakamchagua mmoja wa watu wao mashuhuri, milionea, aliyefanywa milionea kwa wiski na takataka, na upuuzi wa ulimwengu, jinsi alivyofanyika milionea, na kumweka kwenye kiti cha enzi cha Ikulu, pamoja na mfumo wa Ukatoliki nyuma yake. Ambaye, hajakuwa huko miezi sita bado, na anathibitisha kwamba hiyo ni kweli.

170 Nalo kanisa la Kipentekoste lilitoka kwa dhehebu, na kuwaita, "baridi na wa kawaida; nao wanawake wao, jinsi walivyofanya; na wanaume, jinsi walivyofanya." Na Pentekoste ikajiundia dhehebu, na kuichukua ile roho na kurudi moja kwa moja ndani yake. Kwa nini? Ili kwamba Kanisa halisi la Mungu liweze kuonyeshwa katika nguvu Zake na katika utukufu Wake. Unalazimishwa kuliamini. Unalazimishwa kulikubali ama kulikana. Utukufu kwa Mungu! Liko mbele zako, wala huwezi kulikana. Inakulazimu kusema "ndiyo" ama "la." Hakuna njia ya kulikwepa. Naam, bwana. Naam, wanalazimika. Hakuna njia za katikati. Ulimwengu mzima hauna budi kulipokea ama kulikana. Na hivyo ndivyo mambo yalivyo siku hizi.

171 Sasa tunaona ya kwamba baada ya Pasaka, Yesu, katika Marko 16, aliwaambia, "Enendeni ulimwenguni kote mkaibuhiri Injili, ishara hizi zitafuata." Naye mwanadamu. . .Mungu basi alilazimisha hiyo hoja kwa watu hao. Iliwabidi kuona watu hao walikuwa na kitu Fulani! Na hilo lilidumu kwa muda wa miaka mia tatu na sita baada ya kifo cha Kristo. Ndipo ni kitu gani kilichoingia Kanisani? Walikuwa ni wakatoliki, hiyo ni kweli kabisa, wakatoliki wa kipentekoste. Neno *katoliki* linamaanisha "ya ulimwengu mzima." Kanisa zima ni la ulimwengu mzima. Nao walikuwa ni wapentekoste.

Basi wao walifanya nini? Walianza kuingia kwenye biashara, wakiwaongoa hao wengine, kuwaingiza ndani. Nao walikuwa na mawazo ya shirika kubwa.

172 Nalo jambo la kwanza, mwajua, katika Biblia, tuliona katika mafundisho yetu wakati tulipozifundisha *Nyakati Za Kanisa*, ya kwamba Yesu alimwambia kabla halijatukia, yapata miaka mia mbili, ya kwamba kutakuwako na fundisho, ama kwanza yangekuwa ni matendo ya Nikolai, halafu hatimaye yawe fundisho. Ndipo wakati yalipofanya hivyo, Yeye alisema, "Ninayachukia!" Basi Pentekoste ilifanya nini? Wenye vyeo wa Kipentekoste, tabaka baridi, waliunda dhehebu na kulifanya kanisa Katoliki, dhehebu mama la kwanza.

173 Maskini walio wachache walilazimika kwenda upande mmoja. Na imekuwa hivyo tangu wakati huo. Waliendelea kwa miaka elfu moja mia tano, na maskini hao wachache wakaponea. Amina!

174 Mtu fulani alisema hivi majuzi, kasema, "Wazia juu ya kanisa Katoliki, ni vita vingapi vikuu limeponea." Ati vita vikuu? Hakika, she—sheria ikiwa upande wake, pamoja na taifa upande wake, siasa zikiwa upande wake!

175 Wazia juu ya maskini Pentekoste hiyo ambayo haikuwa na kitu ila Roho Mtakatifu, bali iliweza kustahimili. Na papa hapa asubuhi ya leo, ni ushahidi ulio hai ya kwamba ingali hai, Nayo itaishi milele. Si dhehebu; waaminio wa Kipentekoste, walio halisi! Hiyo ni kweli.

176 Sasa, baada ya Pasaka, hili lilifanywa, walilazimika kufanya uamuzi. Mwanadamu hana budi kufanya uamuzi, hawana budi kuufanya sasa. (Ninaruka mengi ya matamshi haya.) Hakuna nafasi ya katikati!

177 Nao wana wa Shetani watatiwa muhuri katika siku hizi za mwisho. Kuna wakati sasa, ambao Biblia ilinena habari zake, ya kwamba wote ambao hawakuwa na Muhuri wa Mungu walichukua alama ya mnyama. Nasi tunajua ya kwamba alama ya mnyama ni kutokuamini. Mara ya kwanza . . . "Vema, ungesema alama ya mnyama ilianza wapi?" Katika bustani ya Edeni. Alama ya mnyama na Muhuri wa Mungu zilitumiwa katika bustani ya Edeni. Kweli kabisa. Inatumika kupitia Pasaka, kwa kuwa kifo cha Habili kilimleta Sethi. Hiyo ni kweli. Angalieni.

178 Kaini alikuwa ni mwana wa Shetani. Alikuwa ni mwana wa mnyama ambaye alimdanganya Hawa. Unaweza kuliita chochote utakacho. Yeye alikuwa ni mwana wa Shetani. Naye alifanya nini? Mungu alimtia alama, kisha akamkufuza kutoka Uweponi mwa Mungu. Hiyo ni kweli? Naye akajipatia mke, sio kutoka kwa urithi wa Mungu; bali akajitwalia mke katika nchi ya Nodi, nchi nyingine.

179 Nalo dhehebu lilifanya nini? Liliachana na imani ya kweli ya Kipentekoste wakati lilipounda dhehebu, na likajichukulia mke kutoka kwa dhehebu. Hiyo ni kweli kabisa. Sasa yale liliyofanya: Angalieni jinsi—angalieni jinsi mke huyo wa Kipentekoste

alivyoanza kufanya, na yale anayosema na yale anayofanya, angalia tendo lake. Na kusimama moja kwa moja huko nyuma, na kujaribu kukatilia mbali sasa. Jambo lile lile lililotetea hapo awali, linajaribu kulikatilia mbali, kulizima kabisa, maana linapinga kanuni zake za imani. Kama ilivyokuwa kule. Lakini linalazimika tena kufanya uamuzi. Halina budi kuufanya. Inalibidi kuufanya.

180 Mungu, nisaidie mimi na ndugu zangu ambao watasimama pamoja nami. Tusaidie, Mungu, tusaidie kusimama pale kwa ushujaa. Haidhuru kama ni damu ya mfia imani, simama hapo! "Sina budi kupiga vita, kama itanibidi kutawala, ongeza ujasiri wangu, Bwana."

181 Ninapoona Roho Wake Mtakatifu akitenda kazi miongoni mwa watu na kufanya mambo yale yale, ninajua Yeye ni Yesu Kristo yule yule aliyefufuka! Amina. Hilo latosha, nijuavyo mimi. Mnaona? Amina. Katika Warumi 4:25, mwishoni, akizungumza juu ya Ibrahimu. "Yeye alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, naye alifufuliwa tena kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu."

182 Waefeso 4:30, Roho Mtakatifu ni Muhuri wa Pasaka ya Mungu ambaye unatutia muhuri kwa ajili ya Umilele. Amina. Anatutia muhuri Milele, Roho Mtakatifu wa Mungu! Loo, mna—mna furaha? Mnafurahia Pasaka? Mnafurahia ujuzi huu? Kutiwa muhuri, kufungiwa pamoja na Mungu katika mahali pa siri, kufungiwa pamoja na Mungu kwa neema Yake ya Kiungu, kutiwa muhuri hata siku ya ukombozi wetu. Huo ndio Muhuri halisi, wa kweli wa Pasaka.

183 Tuna muda gani? Adhuhuri, saa sita kasoro dakika tano. Mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaamini? Hebu tuviinamishe tu vichwa vyetu kwa dakika moja.

184 Baba yetu wa Mbinguni, haidhuru ningesema nini, na hata hivyo mwanadamu anapaswa kuamini Neno hili kwa sababu limeandikwa hapa. Ninaomba ya kwamba watu kila mahali watakupokea sasa kama Muhuri wao wa Pasaka, Malimbuko ya ufufuo, wakijua ya kwamba wamepita kutoka mautini kuingia Uzimani; ambapo mauti wakati mmoja yalikanyaga, sasa Uzima unachukua mahali pake. Ninaomba ya kwamba Wewe utalionyesha kusanyiko hili, asubuhi ya leo, ya kwamba Wewe ungali ni Yesu, ya kwamba Wewe ungali Ndiye Yule afanyaye miujiza na kufanya jambo hili. Na tukijua, na ndio kwanza niseme, kama vile ilivyothibitishwa kwa baba Ibrahimu, kwamba Malaika huyo alisimama huku mgongo Wake umeelekezwa kwa wasikilizaji, ama kwa Sara, na kusema yale aliyokuwa akisema na kuwazia. Ee Mungu, tumeliona wakati baada ya wakati! Tumeona lile thibitisho, kuwekwa kwa Mwana, kutolewa kwa Jina. Tumeyaona mambo haya yote yakitendeka, Bwana, nasi tunajua ya kwamba tuko kwenye

wakati wa mwisho. Hii ni Pasaka. Wengi wamesimama, miguu inauma.

185 Na sasa, Baba, yote ningaliweza kusema hayangemaanisha jambo moja ukiisha kunena Wewe, isipokuwa iwe ni kulingana na yale Wewe usemayo. Na ikiwa nimenena Neno Lako, basi, Baba, ninaamini ya kwamba Wewe ni Mungu ambaye atalithibitisha Neno hilo. Ninaomba ya kwamba utalijalia. Jalia Roho Wako, Bwana, aje miongoni mwa watu, na kuwathibitishia watu hili.

186 Wakati tumeviinamisha vichwa vyetu, kila mahali, labda kuna maradhi hapa ndani. Hakuna shaka hata kidogo hapa ndani kwamba kuna maradhi miongoni mwa watu. Ninataka kujua, ni wangapii hapa ndani ambao wanatoka nje ya mji, walio wagonjwa? Inua mkono wako; nje ya mji. Vema, wako tu kila mahali.

187 Vema. Unaweza kuinua kichwa chako. Nitauliza hilo kusudi mpate kuona. Wote walio nje ya mji ambao siwajui, waliotoka nje ya mji na mimi sikujui, inua mkono wako, useme, "Mimi ni mgonjwa." Inueni mikono yenu kila mahali sasa, ili niweze tu kupata wazo la jumla. Kupitia hapa, hapa, papa hapa kwenye kona hii, na huko nyuma kabisa. Vema. Sasa, hii hapa changamoto: Hii ni kweli ambayo nimehubiri? Kama ni kweli, Mungu anawajibika kulitimiza.

188 Kama halitimizi hili, hakuna ufufuo. Kama akilitimiza, ni hakikisho la ufufuo. Inaonyesha ya kwamba Muhuri wa Pasaka, ya kwamba Yeye hajafa, bali Yu hai. Basi kuhukumu hilo kungekuwa ni kukufuru dhidi ya Roho Mtakatifu, na hakusameheki. Sasa, kama Roho Mtakatifu atakuja kwenye mkutano huu . . .

189 Nilikuwa . . . nilidhani labda tungewasimamisha tu watu, bali hatuwezi kufanyiza mstari wa maombi. Angalia hapa, tumesongamana tu hapa, watoto wadogo kote madhabahuni, na kila mahali. Hatuwezi kufanyiza mstari wa maombi.

190 Lakini, angalieni, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Yeye yuko tu mahali pamoja, ama yuko kila mahali? Yeye yuko kila mahali. Sasa ningewezaje kuwajua, ambao mlikuwa mmeinua mikono yenu kwamba siwajui, nanyi ni wageni hapa? Sitaki yeyote wa watu wa maskani, nitawaona baadaye, mnaona. Lakini hao watu tu, ili muone ni watu wa nje ya mji ambao siwajui. Hebu Roho Mtakatifu anene kama ni kweli ama si kweli. Hebu Yeye azungumze, ndipo maneno yangu yatakuwa ni kitu kimoja; na kama ni Neno la Mungu, Mungu atalitimiza Neno hilo.

191 Sasa kumbukeni, Pentekoste, waaminio halisi wa kweli wa Mungu, daima wamekuwa katika uchache. Nao ni kundi ambalo linachekwa na kudhihakiwa; na watu hawataki kuchukua njia hiyo. Wakati walipokuwa Walutheri, Mungu aliwapa

kuhesabiwa haki nao wakateswa, wakadhihakiwa, na hata wakauawa kwa sababu ya imani.

192 Lakini la Luther likaingia moja kwa moja, likajiundia dhehebu baada ya kifo cha Martin Luther. La, Luther hakuliundia kanisa lolote dhehebu. La, bwana. Lakini watu waliomfuata waliunda, kanisa. Wesley kamwe hakuunda chochote. La, bwana. Ilikuwa ni watu waliomfuata. Na sasa, baada ya Wa—Wapentekoste, waliingia, wakaundia dhehebu kile walichotoka kwake. Mnaona?

193 Lakini hapo ndipo tunapofikia, mnaona, tunarudi moja kwa moja kwenye kanuni zetu za imani, naye Mungu . . . Dakika ile ile (Ninaweza kulithibitisha kwa Biblia.), ya kwamba kanisa lolote linalochukua dhehebu, huchukua alama ya mnyama. Sio watu binafsi kanisani, bali mfumo wa kanisa, kwa sababu mfumo wa kanisa ni Katoliki. Katoliki: wakilifanya lote la ulimwengu wote, wanalivuta ndani, kila kitu. Mnaona? Ninaweza kuthibitisha kwa mlango wa 17 wa Ufunuo ya kwamba alikuwa ni kahaba na binti zake walikuwa ni makahaba. Kila dhehebu huchukua . . . huchukua tabia ya kahaba; basi angalieni vile hasa yeye amefanya, vile vile tu kama mama yake alivyofanya. Kwa hiyo yeye ni mwepesi . . . Sio watu kanisani, sasa. Wamethodisti ni watu halisi.

194 Natumaini utapata kanda ambapo Bwana alinena na kuonyesha kile kitakachotukia kwa kanisa hilo kwenye wakati huu mkuu sasa hivi unaotukabili, wakati hukumu inakaribia kuipiga dunia. Basi angalieni kile kitakacholipata kanisa.

195 Lakini kiongozi wake mwanamume alikufa, mwajua. Lakini wakati . . . Yeye alikuwa ni mjane wakati Eliya aliporudi kutoka kwenye safari yake ya nyikani; alikuwa ni mjane. Eliya alitumwa kwake, alifurahi kumsikia nabii huyo wakati huo, baada ya kiongozi wake mwanamume kufa. Mnaona. Dhehebu lake liliwekwa kwenye Baraza la Makanisa, yeye aliona mahali alipokuwa, na yale nabii huyo aliyosema yalipotimia, alikuwa radhi. Mungu angali alimpenda naye nabii akashuka kule na kumdumisha akiwa hai mpaka alipovuka Yordani nayo njaa ilikuwa imekwisha. Naam, ni kweli.

196 Ni picha nzuri jinsi gani ya Kuja kwa Bwana papo hapo katika Eliya. Kamilifu. Basi kumbuka, Ujumbe huu katika siku za mwisho utatolewa na Eliya, nabii; roho yake juu ya kanisa. Kweli. Kweli. Unajua kile neno Eliya linachomaanisha? Vema. Sasa, na tuombe. Na hebu Roho Mtakatifu . . .

197 Ninataka kuwaulizeni ninyi watu jambo fulani. Sasa, mnaona, hivi Mungu ni Mungu aliye hai? Yeye yupo? Basi kama yupo, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Sasa, nikiisha kuzungumza, ni wangapi humu ndani ambao . . . wanaoamini ya kwamba hiyo ni kweli? Kuna yeyote humu ndani angetaka kusema, "Mimi si Mkristo, Ndugu Branham. Ningetaka kuwa.

Niombee"? Siwezi kufanya wito wa madhabahuni hapa, kwa sababu si—siwezi. Inua tu mkono wako, useme, "Niombee." Kuna yeyote jengoni? Mungu akubariki wewe, wewe, wewe, wewe. Hilo ni sawa. Vema. Mungu awabariki, kote, kila mahali. Vema, sawa. Ni vema.

198 Sasa, unayo haki, baada ya ujumbe kama huu, unayo haki kunipa changamoto, na kusema, "Ndugu Branham, umetuhubiria kitu fulani, kwamba katika siku hizi za mwisho ulisema ishara ya mwisho ilikuwa ni wakati Yeye alipofanya, alipoonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu."

199 Nami nilimsikia mhubiri wa Kiyahudi hivi majuzi, alikuwa tu ameninii. . . Nilikuwa. . . Kwa ujumbe wangu juu ya—juu ya kafara ya ndama mwekundu, mtu huyo alikuja na kumpokea Kristo, alitoka kwenye kanisa ambalo lilikuwa limekuzwa kupitia mlolongo wa marabi kwa miaka na miaka na miaka, kwa—kwa miaka mia nne ama mia tano, huko nyuma kabisa, wote ni marabi. Ndipo mtu huyo akausikia ujumbe wangu, akaingia kisiri mkutanoni na kusikia huo "ndama mwekundu," naye akaongolewa nao kwa Ukristo. Basi alisimama kanisani hivi majuzi, na kusema, "Mtu yeyote ambaye hangeamini ya kwamba kulikuwako na Miungu watatu badala ya Mmoja. . . " Alikuwa akiamini katika Mungu mmoja hadi wakati huo. Alirudi nyuma, badala ya kufanya jambo lingine lolote. Alisema wakati Ibrahimu, wakati hao watatu walipokuja huko, hao walikuwa ni Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu waliomjia Ibrahimu.

200 Sasa, ninataka kuliangalia, kuleta tu kitu fulani mnachokumbuka. Wakati Ibrahimu alipowaona hao watatu pamoja, yeye alisema, sio mabwana wangu, bali, "Bwana wangu." Lakini wakati Lutu, ndugu yake wa kimadhehebu, wakati alipowaona wawili wa hao, yeye alisema, "Mabwana wangu." Hiyo inaonyesha mahali ulipo. Unaona? Lutu aliwaita mabwana wake. Ibrahimu akawaita Hao watatu, "Bwana Wangu." Kulikuwako na mmoja Wao tu pale, aliyekuwa Bwana. Hiyo ni kweli. Elohimu.

201 Ndipo basi hao Malaika wawili, ambao hawakuwa kitu ila wajumbe, wakashuka kule; naye Lutu, yule ndugu mkuu wa utatu, alitaka kuwaita mabwana wake. Mwajua, "Karibuni moja kwa moja ndani." Mnaona hali alimoingia maana alikuwa huko chini pamoja na mambo ya ulimwengu? Mke wake, na binti zake wote huko nje kama tu walimwengu wengine, na kanisa lao baridi, la kawaida. Hivyo ndivyo unavyofikia.

202 Huyo Malaika alifanya nini? Alithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Bwana Mungu. Sasa, huyu Roho Mtakatifu ambaye ninanena juu yake sasa, hebu athibitishe ya kwamba Yeye angali ni Bwana Mungu. Hebu athibitishe ya kwamba alikuwa Ndiye.

203 Sasa, ninyi ombeni. Sasa, hivi nyinyi . . .? Hebu niulize tena. Ni wangapi hapa ndani, hebu tuchukue sehemu ndogo tu kwa wakati mmoja, ni wangapi hapa ndani, mnaosema, hapa ndani ambao—ambao ninyi ni wagonjwa, nami siwajui—siwajui, ninyi ni wageni, nanyi mnataka Mungu awaponye? Inua mkono wako. Sasa, hebu tuangalie kupitia kwenye umati huu hapa. Vema. Vema. Sasa, wekeni mikono yenu chini kwa dakika moja tu.

204 Acheni Mungu anene. Sasa, ninainua mkono wangu, siwajui; siwajui. Sasa, kama Yeye angali ni Mungu, hivi hatafanya jambo lile lile? Mwanamke aliyeligusa vazi Lake . . .

205 Baadhi yenu wanawake, ama baadhi yenu hapo uliyeinua mkono wako, kuna mwanamke mahali fulani, ninaamini. Wapi? Maskini yule mama mwishoni. Ungeweza, kuinua mkono wako? Vema. Uliinua? Vema, mimi ni mgeni kwako? Sikujui? Vema.

206 Hebu angalieni tu kama Yeye angali ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wako. Sijawahi kukuona maishani mwangu. Wewe ni mgeni kwangu. Sijui lolote kukuhusu. Mungu anakujua. Na endapo Yeye anaweza kunifunulia kwa Roho Wake Mtakatifu, Kristo aliyefufuka Yule aliyekuja hapa, na kunipa ufufuo wa muda kwa roho yangu, kwamba roho yangu iondoke sasa na Roho Wake aingie, basi kukufanya ujue kama Yeye yu hai ama la. Sasa, sikujui. Huyo ni mimi, mimi na roho yangu, hatukujui. Lakini Yeye anakujua. Lakini anataka kuazima mwili wangu apate kuthibitisha ya kwamba Yeye ni Kristo aliyefufuka. Nina furaha sana kumkopesha Yeye, kumpa Yeye, chochote anachoweza kupata kutoka kwake.

207 Kama Mungu ataniambia wewe upo hapa kwa sababu gani, utaniamini mimi? [Mama huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Utaamini. Una mishipa iliyovimba. Ikiwa hiyo ni kweli, inua mkono wako. Una zaidi ya hiyo; una ngiri. Hiyo ni kweli. Hutoki kwenye mji huu. Umetoka Lima, Ohio. Jina lako ni Bibi Stoddard. Hiyo ni kweli. Mume wako ameketi nyuma yako. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake ni nini? Ana shida ya mgongo wake, anaumwa na mgongo wake. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, bwana. Unaamini?

208 Mtu mwingine hapa chini aliinua mkono wao, chini kupitia hapa. Hapa, mama yule pale. Vema. Sikujui wewe. Huyo ni mume wako aliyeketi karibu nawe hapo. Kitu unachotaka ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Hiyo ni kweli. Vema, mwamini Bwana, usitie shaka hata kidogo.

209 Nimemwona mtu akija kutoka mbali, bali nisingeweza kusema ilikuwa ni wapi. Naam, ni huyu mtu aliyeketi papa hapa, ninamwona sasa. Yeye ni mgeni kwangu, pia. Una shida ya kibofu nyongo, ugonjwa wa uvimbe wa pua. Hutoki hapa. Umetoka Georgia, mahali panapoitwa kama Hubbermill, Georgia. Vema, amini sasa, kisha urudi nyumbani na uponywe.

210 Unaamini kwa moyo wako wote? Kuna mmoja aliyeketi nyuma papa hapa, nyuma, Nuru ile ikisimama juu ya huyo mtu. Wanamwombea mpendwa aliye na kansa, hajaokoka. Amini, kuwa na imani, usitilie shaka.

211 Ninaangalia tu. Um-hum. Ndiyo Hii hapa. Mwanamke aliyekiinamisha kichwa chake, akiomba. Ana tatizo kwenye miguu yake na magoti yake. Sikujui, sivyo? Sisi hatufahamiani, inua mkono wako. Wewe rudi . . . nyumbani kwako ni huko New Hampshire, huko ndiko unakotoka. Amini, naye Bwana atakupa afya.

212 Mama anayeketi kule nyuma akiwa na msichana mdogo, akimwombea; mwenye ugonjwa wa figo, anayeketi huko nyuma kabisa. Ametoka Georgia, pia. Bi. Cason, kama unaamini kwa moyo wako wote! Unalikubali? Vema, basi nenda nyumbani, ukaponywe. Simjui mwanamke huyo, sijawahi kumwona maishani mwangu. Iwapo hatufahamiani, punga mkono wako, mama. Hiyo ni kweli.

213 Huyu hapa mwingine anayeketi papa hapa nyuma, mwanamume. Ametoka Georgia, pia. Simjui, sijawahi kumwona. Bali nimemwona akija huku kutoka kwenye nchi hiyo ya pichi. Kweli. Yeye ana ugonjwa wa ini, hiyo ni kweli, na baridi yabisi. Ameketi moja kwa moja kwenye kiti cha nyuma. Unaamini kwa moyo wako wote, bwana? Vema, rudi ukaponywe.

214 Kuna mtu fulani anayeketi karibu nawe, mama, huko nyuma kwenye safu ya mwisho kabisa. La, si kwa ajili yake. Anamwombea mwanawe. Hiyo ni kweli. Unaamini kwamba Mungu anaweza kuniambia mwanao ana shida gani, mama? Mimi ni mgeni kwako, bali Mungu anakujua. Vidonda, na kurukwa na akili. Wala hayupo hapa; Dayton, Ohio. Endapo hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa amini.

215 Unajua Yeye yu hai? Je, Yeye ni Yesu yule yule jana, leo, na hata milele? Hao hapo angalau watu wanane ama kumi sijawahi kuwaona maishani mwangu. Hiyo ni kweli? Sasa Mungu wa Mbinguni, Yule aliyepo, na awaponye na kuwapa afya, hawa. Vema, inatokana na upako wa Roho Mtakatifu, sio mimi. Hebu Mungu anayeweza kuyatambua mawazo ya niani, na kujithibitisha Mwenyewe kwamba ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, hebu aje mbele na kuwaponya wagonjwa. Yeye ni Mungu milele! Unaamini hilo? Sasa ni wangapi wanaotaka kumwamini sasa hivi, na kumkubali kama Mwokozi na Mponyaji, na kama Mbatizaji na Mfalme ajaye? Katika Jina la Yesu! Loo, Haleluya! Kitu gani? Muhuri wa Pasaka, Muhuri wa Pasaka usiokosea!

216 Ni jambo gani linalofuata? Kule kubadilishwa kwa mwili huu, kumlaki Mwana ajaye. Tutabadilishwa kwa dakika moja, kufumba na kufumbua jicho. Iweni na mihuri yenu yote ya karatasi mtakayo; bali ule Muhuri halisi wa Pasaka ni Roho

Mtakatifu moyoni mwa mwanadamu! Mnaukubali? Mnaamini katika ufufuo Wake? Mnaamini Yeye yu hai milele? Mnaamini ya kwamba Yeye yupo hapa? Sasa mnamkubali kama Mwokozi wenu, kama Mponya wenu, kama Mungu wenu, kama Mfalme wenu ajaye? Mnaamini kwa moyo wenu wote!

217 Wakati leso hizi, nikiziombea. Mungu, katika Jina la Yesu Kristo! Watu wengi huzitia mafuta. Ninaamini walichukua kutoka kwa mwili wa Paulo, leso na nguo, nao wakaponywa. Mnaamini hilo?

218 Sasa ni wangapi zaidi waliopo hapa ndani, wagonjwa? Sasa watu wa maskanini, na wa karibu na jumuiya hii hapa, walio karibu hapa, sasa ninyi inueni mikono yenu, wanaotoka hapa karibu. Sasa mnaamini ya kwamba Yeye yupo hapa? Mnaamini Roho Mtakatifu yupo hapa? Sasa, ngojeni, kwa nini tungojee kitu chochote kingine? Yeye yupo hapa, kwa hiyo hebu tulifanyie kazi! Charlie, unafikiri nini? Amina. Haleluya! Loo, halina budi kutukia!

219 Siwezi kumponya mtu yeyote. Siwezi kufanya hivyo. Hakuna kitu ndani yangu cha kuponyea. Lakini kama mtamkubali Roho huyu aliye juu yangu sasa, kusingekuwako na ibilisi wa kutosha katika jehanamu kukufanya ulitilie shaka tena, nawe huna budi kuponywa. Mimi si Mponyaji; Yeye ndiye Mponyaji. Siwezi kuona maono; Yeye Ndiye Ambaye ananena. Ni mwili wangu tu anaotumia.

220 Sasa Mungu yuyo huyo alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Ni waaminio wangapi walio hapa? Una hakika kwamba wewe ni mwaminio? Vema, Yeye alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Hiyo ni kweli? Sasa wekeaneni mikono moja juu ya mwenzake, na hebu niombe kwa ajili ya kila mmoja wenu. Ee Mungu! Loo, ndugu! Jambo fulani halina budi kutukia. Jambo fulani halina budi kutukia.

221 Ee Muhuri mkuu wa Pasaka, sio nyinyoro katika chungu, bali Nyinyoro katika Bonde. Wewe, ambaye ulinena kupitia kwa mvulana yule hivi majuzi, Wewe umejitokeza kwa Neno Lako. Ulidhihirisha ya kwamba Wewe ni Kweli. Wewe ni Kweli, Bwana. Wewe ni Ufufuo. Ulisema, "Mimi ndimi Ufufuo, na Uzima: yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi: kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Mimi ndimi Ufufuo, na Uzima." "Mimi ndimi"; si "nitakuwa, nilikuwa"; "Ndivyo nilivyo sasa, Ufufuo na Uzima."

222 Yeye aliyefanya miujiza hii Ndiye Ambaye alihubiri Neno hili. Hivi Biblia haisemi ya kwamba Neno la Bwana lilimjia nabii? Ilikuwa ni nani katika zile siku, waliyemwendea, kujua mahali ufunuo wa kweli wa Mungu ulipokuwa? Alikuwa ni nabii. Nao walijuaje yeye alikuwa ni nabii? Kwa sababu alikuwa na

ishara ya nabii, muhuri wa nabii. Nabii ni nani basi? Roho Mtakatifu.

223 Roho Mtakatifu ndiye aliyeliandika Neno, Roho Mtakatifu. Sio mimi! Yeye! Yeye Ndiye! Ndio kwanza niwaambie, Yeye aliuchukua tu mwili wangu. Yeye huuchukua tu ulimi wangu, anayachukua macho yangu, kwa sababu Yeye alijua ningeyasalimisha Kwake, kwa hiyo Yeye alikuja tu na kunifanya nifanye hivyo. Kwa hiyo si mimi! Ni Yeye! Wala si mimi huko nje pamoja nanyi, ni Yeye huko nje pamoja nanyi. Yeye ndiye Ufufuo na Uzima. Loo, Mungu, Mungu; liamini. Loo, enyi watu: Mwaminini. Mwaminini. Yeye yupo hapa.

224 Sasa, ninataka kila mmoja wenu unayesimama hapo, uwe na imani katika maombi yako mwenyewe. Ninawatakeni muwe na imani katika yale nitakayosema. Nitamwomba Yeye awaponye. Nitamwomba Yeye asamehe kila dhambi. Hiyo dhambi ni nini? Kutokuamini.

225 Kama wewe, baadhi yenu hapa hamjawahi kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo; kidimbwi kiko tayari. Na kama hujabatizwa, kitu pekee kilichokuzuia ni kutokuamini. Kwa nini ukikubali tena? Kikatae kitu hicho. Hivi hamwezi kumwona Roho wa Mungu? Hivi hamwezi kuziona kazi za Mungu?

226 Ondokeni kwenye hayo madhehebu. Ingieni katika Bwana Yesu, kisha mrudi katika dhehebu lenu, na kueneza tu Nuru. Usijali, hutakuwa huko muda mrefu sana. Watakufanyia... Itafanya nini? Italifanya kanisa lako mwenyewe kufikia mahali ambapo litalazimika kufanya uamuzi.

227 Nilipotoka kwenye kanisa la Baptisti na kusimama hapa, iliyabidi ma—makanisa kufanya uamuzi, kwa hiyo wakanitupa nje. Hiyo ni kweli. Ninatarajia kufukuzwa tena, na tena, na tena. Lakini siku moja, nitapokelewa, nitakapovuka Yordani. Kweli. Utatupwa nje, bali wakati utakapovuka Yordani, "Kuna wazo moja linalonifurahisha na kuufanya moyo wangu ufurahi, haitanibidi kuuvuka mto huo peke yangu." Hilo ni jambo moja. Siku moja nitashuka kuja mtoni, sitaninii...Atakuwako Mtu fulani kule akingojea...kunisalimia. Nitakuwa tu mwaminifu.

228 Hapa Yeye alizungumza kupitia Neno Lake, Yeye huzungumza kupitia kila kitu, kila kitu kikifanya kazi kikamilifu tu kupitia kwenye Neno. Hakuna mtu anayeweza kusema lolote dhidi yake. Limewekwa mbele za watu. Hivi karibuni sauti hii itanyamazishwa, enyi watu. Nisikieni. Nisikieni. Hivi karibu haitakuwapo, hapa tena. Halitanenwa, ndipo mtashangaa. Lakini wakati mnapoweza kusikia, tiini.

229 Ee Mungu, Wewe uliyeziumba mbingu na nchi, watu hawa wanaombeana. Wakati ulipofufuka kwenye asubuhi ya Pasaka, ulithibitisha ya kwamba Wewe ulikuwa ni Masihi. Ulithibitisha ya kwamba Wewe ulikuwa Masihi kabla hujafufuka. Ulithibitisha ya kwamba ulikuwa, kwa ishara

ya Masihi, ule Muhuri wa Mungu uliokuwa ndani Yako. Ulitiwa Muhuri na Mungu usifanye chochote ila kile Yeye alichosema. Ulikuwa umesema, "Nafanya sikuzote yale yanayompendeza Baba." Hiyo ni kulitii Neno Lake. Kwa kuwa kumpendeza Mungu, hatuna budi kuliamini Neno Lake na kulitii Neno Lake. Halafu basi, Baba, ndivyo ilivyo siku hizi, kwamba kila mwana ama . . . wa Mungu, kila binti wa Mungu, ili kumpendeza Mungu, hana budi kulitii Neno la Mungu. Na, Mungu, tunalitii Neno Lako sasa kwa kuwekeana mikono. Nami ninaliombea kusanyiko hili.

230 Tukiisha kulisikia Neno likihubiriwa, na kuwaona wageni wakiinua mikono yao, tukaona Roho Mtakatifu mkuu akitoka huko nje na kuwaambia mawazo yenyewe ya moyo wao, na kwamba wao ni nani, mahali wanakotoka, kile kinachoendelea, na yote kuhusu hilo, watu wangewezaje kutilia shaka tena? Mungu, hiyo ni thawabu kubwa kwa ajili ya hawa ambao wamesimama asubuhi ya leo kuzunguka kuta za kanisa hili kuu hapa.

231 Huku viungo vyenu vikiuma, na maskini mama wadogo pamoja na watoto wao wachanga, na akina baba, na wazee, na wote, wakingojea, wakiangalia, wakiangalia kuona ishara moja ya Mungu aliye hai. Kisha kumwona Yeye akijitokeza jukwaani, na kuthibitisha ya kwamba Yeye ni Yehova, ya kwamba Yeye ni Yesu, Yule aliyefufuka. "Mimi ni hai milele, na nina funguo za mauti na kuzimu," kwa sababu Yeye alivunja muhuri wake. Alivunja muhuri wa mauti. Akavunja muhuri wa kaburi. Akavunja muhuri wa kuzimu. Akavunja muhuri wa kaburi. Kisha akaufungua muhuri wa kuingia kwenye Mti wa Uzima, na kutubatiza kwa Roho Wake Mtakatifu tukaingia kwenye Mti huo wa Uzima, na kutufanya wana na binti za Mungu, na akatuagiza kuwekeana mikono: "Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Baba Mungu, haina budi kuwa.

232 Ninatamka kwa nguvu za Injili, kwa Mungu wa Mbinguni Yule aliyenichagua na kunituma nikaihubiri Injili, kwa Mungu Yule aliyeliandika Neno, kwa Malaika Ambaye yupo kulithibitisha Neno, ninasema hili kwa sababu ya imani niliyo nayo katika watu, kwamba itambidi ibilisi kumwacha kila mgonjwa aliye hapa ndani, kila mtu anayeteseka, nazo nguvu za Mungu zitawafufua wapate afya njema na nguvu tena, kama kumbukumbu ya ibada hii ya Pasaka. Toka, Shetani. Wewe umeshindwa. Yesu alikushinda miaka elfu moja mia tisa iliyopita, nawe umeshindwa. Toka ndani ya hawa watu, katika Jina la Yesu Kristo.

Vema, Dk. Neville. Amina.

233 Vema, Ndugu Neville. Ni wangapi wenu mnaamini? Inueni mikono yenu. Ni wangapi wanaosema, wanaosema pamoja

na hili: "Mimi sasa nakubali ya kwamba Yesu Kristo, kama Mwana wa Mungu aliyefufuka, Yeye ni Mwokozi wangu, Yeye ni Mfalme wangu, Yeye ni Mponya wangu. Sasa nimepona. Nimeokoka. Nitamwishia Yeye aliyenifia. Nitasimama kutoka hapa katika upya wa maisha, nipate kusonga mbele nikafanye vizuri niwezavyo Kwake. . . kwa ajili Yake Yeye aliyefufuka kwa ajili yangu. Haleluya!" Mungu aliye hai na apewe sifa.

234 Sasa, unaamini kwa moyo wako wote? Wote watakaokubali hilo juu ya msingi wa Upatanisho. . . Sasa kumbukeni, wakati mmoja Shetani alikuwa amekubinya sana, bali Yesu akakivuta kitu hicho chini kama vile kuvuta kapi kutoka kwenye mhindi. Akalishindilia chini; na kile Yeye alichofanya, Yeye alimfichua Shetani. Ndipo wakati alipofufuka kwenye ile asubuhi ya Pasaka (Haleluya!) Yeye alipata ushindi juu ya ibilisi, juu ya maradhi, juu ya mauti, juu ya kila nguvu za adui, naye huyo adui hana nguvu tena. Yeye ni mdanganyifu tu. Endapo anaweza kukudanganya, vema. Lakini kama hawezi kukudanganya, basi hutastahimili udanganyifu wake.

235 Sasa hivi mnaweza kumpokea Roho Mtakatifu. Sasa hivi mnaweza kujazwa na Roho Wake. Sasa hivi mnaweza kuponywa, kama hamtachukua udanganyifu wake. "Yeyote atakaye, na aje apate kuyanywa Maji ya Chemchemi ya Uzima bure." Kama unaliamini, simama kwa miguu yako, kila mmoja wenu. Inueni mikono yenu na mumpokee Roho Mtakatifu na nguvu za kuponya Kwake, katika Jina la Yesu.

61-0402 Muhuri Wa Kweli Wa Pasaka
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org